# Nipashe

Jumanne Agosti 16, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581039

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




Nipashe TESA

Jumanne Agosti 16, 2022

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Misitu ilivyo na umuhimu wa kipekee uwepo wa maji

Ukurasa 13

Serikali inavyomimina upya sekondari kata na wasichana

Ukurasa 12

TEKNOLOJIA

NA ASHTON BALAIGWA, MBEYA

'VIFURUSHI' UGUNDUZI KILIMO

Kuna mpunga supa unaotesa kwenye maji ya chumvi, magadi

■ Ipo 'Edeni' ya matundapori tiba watu, mifugo

WIZARA ya Kilimo iwekeze kwenye utafiti ili kuleta tija kwenye kilimo ni maelekezo anayotoa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anapozindua Maonyesho ya Wakulima na Wafugaji Nanenane Mbeya.

Mojawapo ya wadau wakubwa wa utafiti wa kilimo ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ambao wanafanya utafiti mbalimbali kupitia vituo vilivyoko karibu nchi nzima, kuibua matokeo kwa ajili ya kuwasambazia wakulima ili waboreshe kilimo na kuongeza tija.

Kazi hizo ni pamoja na kutafiti na kuibua mbegu na teknolojia ya kisasa ambazo zinahimili ukame na magonjwa mbalimbali.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, akizungumza kwenye Nanenane Viwanja vya John Mwakangale, Mbeya, anasema maonyesho hayo yanayofanyika kikanda, TARI imepeleka timu ya watafiti wa mazao mbalimbali kutoa darasa kwa wakulima.

"TARI jukumu letu kubwa ni kugundua au kuainisha teknolojia kuanzia mbegu na ubunifu wa mbinu za kilimo bora kwenye mazao yote ya kilimo yanayolimwa nchini huku tukiweka nguvu zaidi katika mazao ya kimkakati."

Anazungumzia uanzishwaji wa vituo vya umahiri (centers of Excellency) kwenye kila kanda akisema.

"Katika maonyesho hayo yanayofanyika katika kanda nane zikiwamo Morogoro, Mbeya, Dodoma, Shinyanga, Kagera na Singida. Huduma mbegu, TARI imeanzisha vituo mahiri kwa ajili ya kutoa mafunzo ...

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo (kulia), akipata maelezo ya watafiti wa kituo cha TARI Kibaha mkoani Pwani, kuhusu aina mpya ya mbegu ya mahindi kwenye Maonyesho ya Nanenane Mbeya. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

wa thamani vituo ambavyo vinatoa elimu hiyo muda wote na sio kusubiri Nanenane."

Anaongeza kuwa katika vituo hivyo, mkulima muda wote atakutana na wataalamu kwenye vituo hivyo kuhudumia wakulima kuhusu mbegu bora, kupima udongo, matumizi ya mbolea na kuwaelekeza dawa za kutibu udongo uliochoka.

Anaongeza kuwa uanzishwaji wa vituo hivyo mahiri umelenga kuwasogezea huduma karibu zaidi wakulima kwa ajili ya kujifunza teknolojia zilizogunduliwa na watafiti kwenye mazao yote ili kuongeza fursa ya kuongezea tija kwa kutumia mbegu na teknolojia za kisasa zaidi ambazo zimegundulika.

VIFURUSHI UGUNDUZI

Katika maonyesho hayo, Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Dakawa kilichoko wilayani Mvomero Morogoro ambacho kinafanya utafiti wa mpunga, Dk. Jorome Mghase, anazungumzia mafanikio ya kilimo cha mpunga.

Anaelea kuwa, wamefika Nanenane na teknolojia ya mbegu mpya za mpunga, ambazo ni mkombozi kwa wakulima wa zao hilo na kwamba walioacha kilimo hicho kutokana na mashamba yao kuongezeka chumvi, magadi na changamoto ya wadudu pamoja na mabadiliko ya tabianchi watarejea mashambani.

Anawahakikishia kwamba, hivi sasa watarudi katika kilimo hicho kwa tija na watakifurahia baada ya kugundua mbegu za mpunga za'Sato1, Sato9' ambazo zinahimili ardhi yenye chumvi na magadi wakati, TARI Ric1, TARI Ric2 na Komboka zina uwezo wa kukabiliwa na mabadiliko ya tabianchi pamoja na wadudu waharibifu.

Anasema teknolojia ya mbegu hizo imefanyiwa majaribio katika maeneo saba yanayolimwa mpunga kwenye ikolojia tofauti na zimeonyesha kuleta tija na kuongeza uzalishaji wa zao mpunga.

MATUNDAPORI TELE

Mkurugenzi wa Kituo cha TARI -Tumbi cha Mkoani Tabora, Dk Emmanuel Mrema, anasema wamefanya utafiti na kubaini kuwepo kwa zaidi ya aina 50 za miti ya matunda pori kwenye misitu ya miombo hapa nchini yenye uwezo wa kuchangia usalama wa chakula endapo Ikolojia yake itaendelezwa.

Anasema, miti hiyo ya matundapori imebainika kuwa na uwezo wa kutoa lishe na tiba ya kumaliza tatizo la udumavu na kutaka wakulima na wananchi kujitokeza

INAENDELEA UK. 14


UKURASA 11



BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,023,154,178/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




## Kunguru walileta kusafisha mazingira sasa wageuka kero


UKURASA 4


TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



## UCHAGUZI KENYA

# NI RUTO

• **Asema** hatolipiza kisasi, Mwenyekiti Tume ni shujaa...


*Endelea ukurasa 2 & 19*


## YALIYOMO


**UKURASA WA 7**

### WASISITIZA MABADILIKO SHERIA YA HABARI

WADAU wa habari nchini wamesema wanapigania mabadiliko ya Sheria ya Habari kwa...

**UKURASA WA 7**

### WARATIBU WAASWA KUJIWEKA KANDO FEDHA ZA SENSA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella, amewaonya waratibu wa Sensa ya Watu...

**UKURASA WA 8**

### ATCL KWENDA NIGERIA, GHANA MWAKANI

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL), linatarajia kuanza kufanya safari za kwenda nchi za...


## H'mashauri Kuu NCCR-Mageuzi 'yapindua meza'


UKURASA 3




Amiri Jeshi Mkuu, Rais Samia Suluhu Hassan, akipanda mti mbele ya Jengo la Ofisi za Chuo cha Jeshi la Uhamiaji Boma Kichakamiba Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga, alipowasili Chuoni hapo kwa ajili ya kufunga Mafunzo ya Awali ya Askari 820 wa Jeshi la Uhamiaji jana. **PICHA: IKULU**

# Samia anusa rushwa Uhamiaji


**MICHEZO** YANGA: NI USHINDI TU LEO UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu (kushoto), akisaidiana kukata keki na Mkuu wa Uendeshaji wa Matawi ya benki hiyo, Eugene Massawe, katika hafla fupi ya kusherehekea maadhimisho ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa benki hiyo iliyofanyika makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam jana. Massawe ni mmoja wa watumishi wa benki hiyo waliohudumu kwa kipindi cha zaidi ya miaka 20. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ruto atangazwa Rais wa Kenya

**Na Elizabeth Zaya**

NI kutoka kuuza kuku, Naibu Rais hadi kutangazwa kuwa Rais wa Kenya kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, Dk. William Ruto.

Alitangazwa kuwa mteule wa kiti cha urais baada ya Wakenya kufanya uamuzi wa kumchagua kwa kura zaidi ya milioni 7.17 sawa na asilimia 50.49 dhidi ya mshindani wake mkubwa, Raia Odinga aliyepata kura milioni 6.9 sawa na asilimia 48.8. ya kura zote zilizopigwa.

Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC), Wafula Chebukati, ndiye aliyetangaza matokeo hayo jana saa 11:05 jioni baada ya kusubiriwa kutwa nzima.

Kabla ya kutangazwa kwa matokeo hayo palitokea purukushani ikiwamo baadhi ya watu kunyanyua viti hali iliyofanya baadhi ya waangalizi kuondoka ukumbini humo.

Kabla ya matokeo hayo, Chebukati alisema, aliamua kufanya hivyo kwa kulinda nchi yake na kuheshimu katiba ya nchi licha ya purukushani alizopata kuifikia uamuzi wa kufanya hivyo.

"Nimeondoka ofisini kwangu kuja kutangaza matokeo haya, kusaidia nchi yangu na kulinda katiba ya nchi yangu, lakini Wakenya watambue kwamba tunahitaji tume huru ya uchaguzi," alisema Chebukati.

"Najivunia kufanya kazi hii kwa uaminifu na bila woga na huu utakuwa uchaguzi wangu wa mwisho."

"Nawashukuru wote walioshiriki katika kufanikisha uchaguzi huu licha ya kuwamo Jeshi la Polisi, wanadiplomasia manyanyaso waliyopata hapa Bomas na maeneo mengine, kuna maofisa wa tume 12 wamejeruhiwa wanaendelea na matibabu, sita wameondoka kwenye vituo vyao hawajulikani waliko," alisema Chebukati.

'Ngoma ilikuwa nzito' wakati wa kutangaza matokeo hayo ambayo awali yalikuwa yatangazwe saa tisa alasiri kama ilivyokuwa imeahidiwa na tume hiyo, lakini yakatangazwa saa 11:05 jioni.

**MAKAMISHNA WAKATAA MATOKEO**

Wajumbe wanne wa Tume hiyo wakiongozwa na Naibu Kamishna Juliana Cherela, waliitisha mkutano na waandishi wa habari hoteli ya Serena na kusema kuwa hawakubaliani na matokeo yatakayotangazwa kwa madai kuna taratibu zimekiukwa.

Aliambatana na makamishna watatu na hakutoa nafasi kwa waandishi wa habari kuuliza maswali na kuahidi kutoa taarifa ya kina ndani ya siku mbili.

"Tumefanya kazi nzuri na kwa ufanisi kwa upande wetu katika uchaguzi huu, lakini hatutakuwa sehemu na hatukubaliani na kile kitakachokwenda kutangazwa," alisema Juliana.

**WAFUASI WA ODINGA**

Nje ya Bomas wafuasi wa Odinga walisikika wakisema uchaguzi huo ni mbovu na kwamba nchi hiyo haijawahi kupitia hali kama hiyo huku wakitaka matokeo yanayotangazwa kuwa ni yale yaliyohakikiwa.

Baada ya hali ya vurugu kutulia, Ruto aliingia ukumbini humo na Askofu alikaribishwa kuongoza sala ambaye kabla ya kusali alisema: "Tuweke kando tofauti zetu, watoto waende shule, tunataka amani ya nchi yetu, tuheshimu katiba yetu na maamuzi ya wananchi."

**SITALIPIZA KISASI**

Akizungumza baada ya kutangazwa kuwa rais mteule wa Kenya, Ruto alimshukuru Mungu kwa uchaguzi huo huku akisema wananchi wa Kenya wamefanya kwa mujibu wa Katiba kwamba madaraka yako mikononi mwao.

"Namshukuru Mungu, leo tumemaliza huu uchaguzi, najua kulikuwa na utabiri kuwa sitapata kura za kutosha, tusingefika hapa bila Mungu, tumefika kwasababu kuna Mungu wa mbinguni anayetushindia ndiyo maana tuko hapa, bila Mungu tusingekuwa hapa," alisema na kuongeza:

"Asante zangu zinakwenda kwa Wakenya wanaotusikiliza, walishiriki kwenye kampeni zetu kwa ustaarabu, waliojitokeza kupiga kura Agosti 9, mwaka huu."

"Mamilioni waliosubiri hadi tangazo hili (mshindi) limetolewa...huu uchaguzi ulikuwa ni muhimu kuliko mahali tunapotoka, shukrani ziwaendee Wakenya wote waliotumia haki yao ya kikatiba kuchagua bila kujali eneo tunalotoka," alisema.

Alisema kwenye uchaguzi huo hakuna aliyeshindwa bali Wakenya wameshinda na kwamba kila aliyeshiriki ni mshindi.

"Washindi wa uchaguzi huo ni IEBC iliyoongozwa na Wafura Chebukati, nasema haya kwamba wametushangaza kwa matokeo kuwa wazi kwenye mtandao, kila kitu kilikuwa wazi na kila aliyehitaji kujua alitakiwa kujumlisha, nawapongeza sana. Jasiri wetu ni Chebukati, anaongea taratibu, lakini ana msimamo," alisema Ruto.

Alimshukuru mshindani wake wa karibu Odinga kwamba wakati wa kampeni walizungumzia ajenda za Wakenya na kuahidi kufanyakazi pasipo kumwacha yeyote kando.

Pia alimshukuru Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta ambaye alifanya naye kazi kwa miaka 10 serikalini, huku akiahidi kuendeleza yote waliyoyafanya kwa ajili ya Wakenya na kupeleke mbele nchi kimaendeleo huku akiwaahidi kuwa itakuwa serikali ya wananchi.

Aidha, alisema hatalipiza kisasi kwa yeyote aliyewatendea kinyume na kwamba hakuna nafasi hiyo bali wataangalia mbele, kwa kuwa nchi inawahitaji wote, ili kusonga mbele kwa maendeleo na hakuna yeyote atakayelaumiwa wala kunyooshewa kidole bali kufanyakazi kwa pamoja kuimarisha demokrasia na ustawi wa Kenya.

# Samia anusa harufu rushwa Uhamiaji

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu ameeleza kukerwa na vitendo vya askari wa Jeshi la Uhamiaji wasiokuwa waadilifu wanaochukua fedha za Visa, vibali na kuzigeuza za kwao kwenye vituo vya Zanzibar na Dar es Salaam na kuamuru vitendo hivyo vikomeshwe.

Alitoa agizo hilo jana wakati akifunga mafunzo ya awali ya Jeshi la Uhamiaji kwa maofisa 818 waliyopewa jina la Operesheni Ujenzi katika Chuo cha Uhamiaji cha Boma- Kichakamiba wilayani Mkinga mkoani Tanga.

Alisema vitendo hivyo havipaswi kufumbiwa macho na kutaka vikomeshwe haraka, ikiwamo waliohusika kuchukuliwa hatua ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia hizo.

"Nimesikia kuna maofisa askari ambao sio waaminifu kuna kesi kwenye mafaili sasa hivi fedha zinazotolewa za Visa na vibali wanazigeuza za kwao na wanaweka mifukoni, katika utafiti mdogo uliofanywa mapema mwaka huu hasa pale vituo vya Zanzibar na Dar es Salaam nimegundua upotevu mkubwa wa fedha na Visa ambao unafanywa na maofisa wa Uhamiaji kwa vitendo vya aina hii vikakomeshwe ndani ya jeshi lenu," alisema Rais Samia.

Aliwataka warudi kwenye maadili ya jeshi hilo kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao ipasavyo kwa nidhamu na weledi mkubwa ikiwamo kuhakikisha vitendo hivyo havijitokezi tena.

Alisema maofisa wa Jeshi la Uhamiaji watalazimika kufanya kazi kwa weledi kufuata kanuni na sheria bila kubagua wananchi na wageni wanaokuja nchini kwa kuwa wanapokwenda tofauti wanaleta picha mbaya kwa taifa.

"Mpo hapa leo, lakini mkifika kwenye vituo mnabadilika, nimesikia kwenye kaulimbiu umoja na upendo mshikamano na kukataa rushwa, niwatake mheshimu kwa vitendo kaulimbiu kwenye vituo vyenu kwani tunashuhudia kiasi kikubwa cha kupokea rushwa maofisa Uhamiaji na vitendo vya unyanyasaji kwa wageni wanaoiingia nchini," alionya.

"Huko katika vituo tunashuhudia kiasi kikubwa cha kupokea rushwa kwa maofisa Uhamiaji, tunashuhudia vitendo vya unyanyasaji kwa wageni wanaoingia na malalamiko kutoka kwa wageni," alisema.

Alitaka jeshi hilo kuondoa na kupunguza urasimu wa utoaji wa vibali kwa wageni na wenyeji wanaoingia na kutoka nchini kwa kuharakisha utoaji wa vibali hivyo hali inayolalamikiwa kwa muda mrefu.

"Ningeomba sana punguzeni urasimu kwa aina zote za Visa. Kwa sababu sasa hivi mnatumia teknolojia hakuna sababu ya kuchelewesha watu kupata Viza," alionya.

"Na kwa hivyo maofisa na maaskari wa Jeshi la Uhamiaji mtalazimika kufanya kazi kwa weledi na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizoko bila kuwabugudhi wananchi, wageni na wawekezaji wanaokuja nchini," alisema Rais Samia.

Naye Kamishna Jenerali wa Jeshi la Uhamiaji nchini, Dk. Anna Makakala, alisema kuwa licha ya kuendelea kutoa mafunzo katika chuo hicho bado wanakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo ukosefu wa miundombinu ya kutosha, ofisi na za wilaya pamoja na miundombinu ya majisafi na salama na kumwomba kuliangalia jeshi hilo kwa jicho la pekee.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamadi Masauni, alimshukuru Rais Samia na serikali baada ya jeshi hilo kupata mafanikio makubwa ndani ya muda mfupi toka alipoingia madarakani.

Alielezea Idara ya Uhamiaji kupata hadhi ya kuwa jeshi ni jambo kubwa ikiwa ni pamoja na kupokea stahiki za kijeshi na kutunukiwa nishani kwa maofisa na maaskari jambo ambalo ni la kihistoria na limeongeza ari ya kufanya kazi na uwajibikaji.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba, alimwomba kiongozi huyo kuzungumza na viongozi wenzake wa nchi jirani ili kutekeleza sheria za kimataifa.

Alisema mkoa huo una mahabusu na wafungwa wa nje ya nchi 946 huku zaidi ya 853 wakisubiri kurudi kwenye mataifa yao ambayo yatafanya juhudi zozote za kuwachukua.

Mgumba alisema katika mkoa huo pia kuna baadhi ya Watanzania ikiwamo watumishi wa umma wanaojishughulisha na biashara ya kuuza wahamiaji haramu kutoka nchi jirani kwa Sh. 150,000 na kwenda kuwauza kwenye mikoa mingine ili kuwasafirisha wanakoelekea.

# Halmashauri Kuu NCCR-Mageuzi yapindua meza

**Na Jenifer Gilla**

HALMASHAURI Kuu ya Chama cha NCCR-Mageuzi, imeazimia mambo 14 ikiwamo kumvua uongozi Katibu Mkuu Martha Chiomba.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Idara ya Uenezi na Uhusiano wa Umma wa chama hicho, Edward Simbeye, alisema tayari imeshawasilisha maazimio hayo kwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa ajili ya utekelezaji.

Simbeye alisema kikao cha Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi kilichofanyika juzi, pamoja na mambo mengine kilitengua uamuzi wa kumvua uenyekiti, James Mbatia na Makamu Mwenyekiti Bara, Angelina Mtahiwa.

"Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi imeelekeza sasa warudishe mamlaka ya ofisi kwa viongozi hawa halali, kwa hiyo Baraza la Wadhamini wa Chama litaandika barua leo ili zipelekwe kwenye zile taasisi zote, sasa viongozi halali ni hawa na sisi tunaruhusu ofisi hizi zitumiwe na viongozi hao," alisema.

Alisema hatua inayofuata ni kuwaita viongozi hao katika kamati ya maalum ya chama iliyoundwa na Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi ili kuwapa nafasi ya kujitetea kwa nini wasifukuzwe uanachama kutokana na vitendo walivyovifanya.

Alisema kuwa kitendo cha Martha kupingana na maamuzi ya halmashauri kuu ya chama hicho hakina tija kwa sababu halmashauri hiyo ndiyo imemchagua yeye na ndiyo inamamlaka naye.

"Inapomwambia umeshindwa kuendelea sasa kaa pembeni halafu akisema hutaki ama hutambui ni sawa na wewe leo kusema kuwa humtambui mama yako aliyekuzaa, kwa hiyo unaposema hutambui, hutambui nini?" Alihoji.

Martha alipotafutwa juzi na vyombo vya habari kuzungumzia uamuzi huo alisema angezungumza na wanahabari katika ofisi za makao ya chama hicho.

Hata hivyo, Nipashe ilipofika katika ofisi hizo ilifahamishwa kuwa atazungumza na waandishi wa habari baada ya kufanyika vikao vya ndani.

Wengine waliovuliwa vyeo vyao kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo za kutumia vibaya madaraka yao ni Haji Ambar Khamis, Ameir Mshindani, Susan Masele na wajumbe wote waliosababisha mgogoro ndani ya chama hicho.

Mei 22, mwaka huu, Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi iliwasimamisha uongozi Mwenyekiti wa chama hicho, James Mbatia na Makamu wake Tanzania Bara, Angelina Mtahiwa, kutojihusisha na shughuli za chama kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo ukiukwaji wa maadili, kuwagombanisha viongozi wa chama hicho na kuwalazimisha wasaini kujiuzulu.

## Ma-DC wilaya mpya waionavyo sensa

**Na Beatrice Moses**

WAKUU wa wilaya mpya nchini wamesema kwa miaka saba bajeti kwenye wilaya zao zinatekelezwa kwa makadirio bila kuwa na idadi sahihi ya wakazi.

Wanaamini sensa itawasaidia kupata idadi sahihi ya wakazi kwenye maeneo yao, hatua itakayowezesha kuboresha huduma za kijamii.

Walikuwa wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kuhusu umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu, ambayo kwa wilaya hizo ni mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam, Heri James, alisema sensa itasaidia serikali kupanga bajeti kwa kuzingatia idadi sahihi na mahitaji badala ya makadirio yasiyo sahihi ambayo yanachelewesha kasi ya maendeleo.

"Sisi ambao ni wilaya mpya yapo mahitaji ambayo tunayaomba, lakini kwa sababu hakuna viashiria halisi kwa sababu hakuna takwimu sahihi tunafananishwa na wilaya nyingine kongwe, hii sensa itasaidia serikali kutuhudumia," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, Onesmo Buswelu, alisema sensa itawezesha kupata bajeti inayolingana na mahitaji halisi badala ya kukadiriwa pamoja na kuwa na mgawanyo sahihi wa huduma utakaoongozwa kulingana na idadi ya watu.

"Mfano sisi tuna shule za msingi 81 kwenye vijiji 55 kati ya hizo, shule 24 ni mpya, kwa kuwa lengo la sensa ni kutambua makazi, vizazi na vifo ili kujua wapi nguvu zielekezwe zaidi katika kuboresha huduma ikiwamo za afya, elimu na miundombinu," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam, Fatuma Nyangasa, alisema sensa itasaidia kuipanga vizuri wilaya zaidi hasa ikizingatiwa kuwa wilaya hiyo ina eneo kubwa la uwekezaji, itasaidia kuendelea kujengwa kwa kuzingatia mpango miji na sio kiholela, tatizo ambalo linazikabili wilaya nyingine kongwe.

"Kuna maeneo tayari yametengwa kwa ajili ya masoko na sasa tunatafuta fedha ili kuyajenga, hapo wananchi watapata huduma pia wale wafanyabiashara watafanya kwenye maeneo rasmi," alisema.

IITA
Transforming African Agriculture

ILRI

**POSITION ANNOUNCEMENT**

**RANGELAND ECOLOGIST**

**IITA-TZ-2022 - R4D-009 -NRS-DSM**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Livestock Research Institute (ILRI) invites applications for the position of Rangeland Ecologist. The Rangeland Ecologist will provide support to local Scientists, Government including the Ministry of Livestock and Fisheries, NGO and communities in implementing participatory rangeland management plans and rangeland restoration in central Tanzania.

The successful applicant will join the Sustainable Livestock Systems program of ILRI and will contribute to the One CGIAR initiative Livestock, Climate and System Resilience (LCSR) which seeks to improve understanding on how to develop and strengthen resilient, low-emission livestock agri-food systems.

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in in Kabaya town, Kiteto district, Manyara region- Tanzania, with anticipated occasional travel to other pastoral areas.

**Roles and Responsibilities:**
- Coordinating the undertaking of a physical baseline in action-research intervention areas using LAND PKS and participatory community data collection tools,
- Ongoing monitoring of ecological changes,
- Establishment of action-research trials on rangelands restoration with communities, trainings of stakeholders as required, and liaison with government, NGOs and other researchers
- Facilitating visits and research being undertaken by ILRI scientists and partners.

This work will be embedded in a participatory rangeland management (PRM) approach, that ILRI and partners have developed and which is in the process of being scaled-up. It is also anticipated that the ecologist will play a role in influencing a more enabling policy environment for PRM and engage with the private sector to develop partnerships for investment in rangeland restoration and/or payments for ecosystem services.

**Qualifications and Experience:**
- Master degree in rangeland ecology, dryland ecology, agriculture or related subject.
- At least two years working as a rangeland ecologist in pastoral areas of Tanzania including in rangeland restoration.
- Proven training and community facilitation skills.
- Experience in participatory or community-based rangeland management and monitoring.
- Experience in participatory land use planning an advantage.
- Knowledge of remote sensing an advantage.
- Fluent in written and spoken English and Swahili, and knowledge of Maa an advantage.

**General information:**
The duration of contract for the position is two years. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.**

Female applicants are strongly encouraged to apply.

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

216989101

# Kunguru waliletwa kusafisha mazingira sasa wageuka kero

**Na Halfani Chusi**

KUNGURU, jina maarufu kunguru wa Zanzibar ambao waliletwa nchini kutoka nchini India kusaidia kuokota taka maeneo mbalimbali, sasa wamegeuka kero kwa jamii, kuchafua mazingira na kuharibu miundombinu ya umeme.

Kwa wakazi wa Dar es Salaam, ongezeko la ndege hao maeneo ya makazi, sehemu za biashara hususan ya chakula wanasababisha uharibifu wa miundombinu ya umeme na baadhi ya maeneo kukosa nishati hiyo.

Ndege hao wanapatikana Dar es Salaam na Zanzibar na huanza harakati zao alfajiri kwa kelele za milio yao.Wana rangi nyeusi na macho makubwa ya wastani tofauti na kunguru waliozoeleka kuonekana siku za nyuma wenye baka jeupe kifuani ambao kwa sasa ni adimu kuonekana.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe umebaini kuwa ndege hao wameongezeka kwa kasi na kuwa kero kwa wananchi na kuharibu miundombinu.

Mtu asipokuwa makini hudonoa macho ya mtoto mchanga kama hatakuwa chini ya uangalizi anapowekwa nje na vile vile hubeba vifaranga vya kuku, viota vya ndege na kuharibu mayai kwa kuyadonoa.

Mwili wa ndege huyo unaelezwa kuwa sumu hali inayofanya ndege wengine kuwaepuka kuwala.



Kunguru mweusi maarufu kunguru wa Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

**WAJASIRIAMALI WAZUNGUMZA**

Mwajuma Ali, mjasiriamali anayeuza chakula eneo la Sinza kwa Remy, jijini Dar es Salaam, anasema amewahi kupata hasara kubwa kutokana na ndege hao kubeba nyama aliyokuwa amenunua kwa ajili ya kupika siku hiyo.

“Siku moja nimetoka sokoni nikaweka nyama niandae kwa ajili ya wateja wangu, wakati naosha vyombo waliteremka kunguru wengi wakadonoa hadi ikaisha nakuja kushtuka imekwisha,” anasimulia.

Muuza chips, kutoka eneo la Tabata, Babu Ali, anasema kunguru walidonoa mayai aliyokuwa ameweka juu ya meza ya kuuzia chips, jambo ambalo lilimpa hasara kubwa.

“Siku moja niliyaacha mayai hapa nikaenda gengeni kununua nyanya kwa ajili ya kachumbari niliporudi nikakuta mayai karibu yote yamedonolewa, nilishindwa kuendelea na biashara kwa kuwa mtaji wangu ulishamegwa, nilipata hasara sana.”

Mfanyabiashara mwingine wa genge, Ramadhani Malenda, anasema ana genge lake, akitoka kidogo anakuta nyanya zimedonolewa na nyingine zikiwa chini na kwamba wafanyabiashara muda wote wanapaswa kuangalia bidhaa zao vinginevyo zinabebwa.

**KERO NYUMBANI**

Kunguru hao huvizia hata chungu kilichobandikwa jikoni na kubeba chochote kilichomo ndani.

“Siku moja nilinunua samaki wabichi nikawaosha nikawanika ili niwakaange, nilipogeuka sikukuta hata kipande kimoja, familia yangu ilipata hasara kubwa, sikuwa na fedha ya kununua nyingine tulikosa mboga kwa siku hiyo,” anasema.

Sada Mtarula, anasema waliondoka na nguo yake ya ndani aliyokuwa ameanika kwenye kamba na kuruka nayo juu ya mti.

“Nikajaribu kumrushia mawe, lakini haikusaidia akapaa juu kuelekea sehemu nyingine na nguo yangu mpaka leo sijaipata tena nilifikiria sana hadi nikahisi labda atakuwa ametumwa yule kunguru,” alisema.

Pia kunguru hao wanaelezwa kuwa na tabia ya kubeba vitu ving’aavyo kama pete, hereni, simu za mkononi, vijiko, visu, vipande vya chuma na vitu vyenye harufu.

Aidha, wananchi wamelalamikia kuharibiwa antena za ving’amuzi na waya zinazounganishwa na ungo wa televisheni.

Kadhalika hupenda kujisaidia kwenye nguo nyeupe na kutua kwenye vichwa vya watu walionya kipara na kuwadonoa.

**UHARIBIFU MIUNDOMBINU**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema kunguru hao wanafanya uharibifu mkubwa wa miundombinu na kusababisha wananchi kukosa nishati hiyo.

Meneja Mwandamizi wa Kanda ya Mashariki wa TANESCO, Kenneth Boymanda, anasema ndege huyo ni adui namba moja wa miundombinu na uhakika wa nishati hiyo.

“Kunguru wamekuwa wakituingiza katika hasara za mara kwa mara kwenye miundombinu ya umeme huwa anasababisha kukatika kwa umeme, wakati mwingine huwa anasababisha hitilafu kwenye mkondo wa umeme.

Anasema kunguru wanapenda kutua kwenye nyaya za umeme na wanapotaka kuruka mbawa zikigusa mkondo wa juu na chini husababisha umeme kulipuka.

Boymanda anasema ndege hao hujenga viota kwenye miti kwa kutumia vipande vya vijiti na nyaya na kwamba akishaokota kipande cha waya akienda kusimama kwenye waya wa umeme, akigusisha na waya wa mkondo wa umeme anaweza kusababisha shoti ya umeme au kukosekana umeme kwa saa kadhaa mpaka mafundi watakaporekebisha.

“Kunguru wamekuwa wakitia hasara sana kwenye miundombinu ya umeme mfano umeme unapo katika kwenye mkondo wa megawati 10 kwa saa moja unapoteza uniti Sh. 10,000 ambayo ukipiga hesabu ni zaidi ya Sh. 2,920,000 kwa saa moja,” alisema na kuongeza:

“Kimahesabu kama kwa saa umeme ukikatika unasababisha hasara ya Sh. 2,920,000 ikijitokeza mara nne kwa mwezi ni Sh. 11,680,000 kwa mwaka tunapoteza Sh. 140,160,000 hapo ni umeme unapokosekana kwa saa moja. Ni kwa namna gani hapo utaona serikali inapoteza mamilioni kutokana na uharibifu unaofanywa na kunguru.”

Kuhusu mbinu zinazotumika kukabili hali hiyo, anasema: “Kwa sababu kunguru wanapenda sana kukaa maeneo ya kutupa taka huwa tunahamisha dampo zilizopo karibu na mkondo wa umeme, lakini njia nyingine huwa tunavisha magamba magumu yaliyoko katika mfumo wa plastiki kwenye nyaya za umeme, ili isiwe rahisi kusababisha hitilafu.”

**JINSI YA KUWADHIBITI**

Mtaalamu wa uhamasishaji wa wanyamapori na ndege Dar es Salaam Zoo, Sekunde Mbwambo, anasema: “Zipo njia nyingi za kudhibiti kero ya kunguru katika jamii kwa kuwa na mtego ambao umetengenezwa kwa mfumo wa pipa na kuweka chombo ambacho kunguru wakisimama juu wanatumbukia na mfuniko unajifunga.”

“Hii mitego ipo wilayani kote ukiona eneo ulipo kuna usumbufu mkubwa unaenda kuchukua unawatega na wakiona wanapungua wote wanakimbia kwa sababu ni waoga sana.”

**TABIA ZAO**

Kamishna Msaidizi mstaafu wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Marco Meoli, anaeleza; “Mwili wa kunguru umejaa sumu nyingi sana hivyo sio rahisi kwa ndege mwingine kumla, lakini ana tabia ya kudonoa macho ya watoto wachanga kwa hiyo sio vizuri kumuacha mtoto mchanga peke yake kwenye mazingira yenye kunguru.

Anasema sifa ya kunguru ni kivutio cha utalii kwa sababu kuna baadhi ya watu hasa wa vijijini sana hawajawahi kumwona.

Pia, kunguru ana maamuzi ya haraka sana, na ana macho yenye uwezo mkubwa wa kuona, anaonekana kuwa na ujasiri mkubwa hamwogopi binadamu tofauti na ilivyo kwa ndege wengine.

Ana uwezo wa kumtambua binadamu mwenye nia mbaya na nzuri dhidi yake na anatajwa kuwa ni kati ya ndege wenye machale sana kuhisi hatari kwa haraka zaidikushinda ndege wengine wote.”

**NINI KIFANYIKE**

Mstaafu huyo anaishauri serikali kuwapo na utaratibu wa kuhamisha magenge ya kunguru kwa kusambaratisha maskani yao kama mti ambao huwakutanisha, ukatwe hapo unakuwa umewahamisha eneo hilo.

Anasema maskani nyingine ya kunguru ni sehemu zinaporundikwa taka kwamba kuna haja ya kuangalia namna bora ya kuzihifadhi ili kutowaruhusu kufika eneo hilo.

Pia, namna bora ya kuwapunguza kwa kushirikiana na mamlaka inayohusika na ndege, pamoja na kuwahamishia sehemu nyingine kwa kuwa huku wameletwa na wanaweza kuwapelekwa sehemu nyingine.

**HISTORIA YAO**

Mtaalamu kutoka kampuni inayojihusisha na uhamasishaji wa wanyamapori na ndege Dar es Salaam Zoo, Sekunde Mbwambo, anasema kunguru waliletwa na Serikali ya Uingereza visiwa vya Zanzibar mwaka 1890 wakitokea India kwa lengo la kusaidia kupunguza taka.

Baada ya hapo kunguru hao walizaliana kwa wingi na kufika Pwani ya Dar es Salaam, kati ya mwaka 1950-1955 kwa njia ya majahazi na meli na kusambaa katika mikoa mingine kama vile Pwani, Lindi, Morogoro, Tanga na Mtwara.


AJ RECOVERIES LTD
Your vision our future

AJ RECOVERIES LIMITED|REG:141077236|Shekilango sokoni|Ubungo | P. O. Box 1056 | Dar Es Salaam |Tanzania, (Mobile) +255 686153126 : (Mobile) +255 746 336875| Directors: ALEX C.KAMUZELYA(Tanzanian), JOHN MWAKASONDA(Tanzanian).

## TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **LETSHEGO BANK (T)LIMITED– TAWI LA MANZESE** , tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wa benki ya **LETSHEGO BANK** ili kufidia deni lake;

| S/NO | JINA LA MDAIWA | TAWI | DHAMANA | MAHALI ILIPO | SIKU NA TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KHAIFY TRADING COMPANY LIMITED | MANZESE | GARI, TOYOTA DYNA WITH REG. NO. T 913 DES | OFISI YA LETSHEGO BANK TAWI LA MANZESE | JUMANNE 31/08/2022 SAA 03:00 ASUBUHI |
| 2.. | KHAIFY TRADING COMPANY LIMITED | MANZESE | GARI, SCANIA 92 HWITH REG NO. T 790 DFU | YARD, KIMARA TEMBONI | JUMATANO 31/08/2022 SAA 6:00 MCHANA |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi atalipia asilimia 25% ya bei ambayo imefikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki anatakiwa kumaliza ndani ya siku kumi na nne(14), endapo atashindwa kumalizia salio lililobaki mnada utarudiwa upya na fedha iliyolipwa haitarudishwa. Ukaguzi wa dhamana ni kwa kuwasiliana na dalali au Tawi la benki ya manzese, siku yoyote muda wa kazi.
2. Gharama za kubadilisha umiliki wa dhamana ni ya Mnunuzi.
3. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo.

116994801

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Fursa hii ya mikopo kuanzisha vituo vya mafuta ichangamkiwe

**TAARIFA** kwamba, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kuwadhamini watu wanaotaka kuanzisha vituo vya kuuza mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa vijijini zitasaidia kuepusha majanga ya moto kwenye makazi ya watu.

Juzi wakala huo ulitoa taarifa kuwa uko tayari kudhamini watu hao kupitia mikopo itakayotolewa na benki ili kuwawezesha kuanzisha vituo hivyo.

Katika taarifa hiyo ilielezwa kuwa, zaidi ya Shilingi bilioni mbili zitakopeshwa kwa wananchi wanaotaka kuanzisha vituo hivyo maeneo ya vijijini, ili kuhakikisha usalama wa watu na bidhaa yenyewe kwa vyombo vya usafiri na mitambo.

Wakala huo umesema, kwa sasa wanakamilisha taratibu za kutoa mikopo hiyo na kuwatambua waombaji, maeneo yatakayowekwa vituo na kuhakikisha tathmini ya uharibifu wa mazingira imefanyika.

Tangu kuanzishwa kwa REA mwaka 2007 zaidi ya Shilingi trilioni tatu zimetumika kusambaza nishati hiyo vijijini, pia kuchangia ukuaji wa uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na maendeleo vijijini kwa asilimia 25.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidi na Mkurugenzi wa Uendeshaji Masoko na Teknolojia, Advera Mwijage, wakati wakizungumzia majukumu, changamoto na mafanikio ya wakala tangu kuanzishwa kwake, walihakikisha wananchi kuwa wamefikia uamuzi huo kutokana na mwenendo wa uuzaji mafuta vijijini ambao ni holela na hatarishi kwa maisha ya watu na kuharibu vyombo vya usafiri na kwamba utaratibu utakaotumika ni kuwaunganisha na benki ziwakopeshe.

Uuzaji wa nishati hiyo katika maeneo mbalimbali hasa ya vijijini ni kuweka kwenye magaloni ndani ya nyumba ambako ni hatari kama yatakuwa karibu na moto na kulipuka.

Katika baadhi ya maeneo pia, uuzaji huo hutumika kwa kuwekwa kwenye chupa za maji zilizotumika na kupangwa barabarani huku zikipigwa na jua, hali ambayo pia ina hatarisha usalama wa watu na pia kupunguza thamani ya bidhaa yenyewe.

Viongozi hao waliwataka wananchi wauze mafuta kwa utaratibu mzuri na usafi na lengo la kuja na mpango huo wa mikopo ni kuwadhamini kwa mwaka huu wa fedha.

Fursa hii ilitolewa na REA haina budi kuchangamkiwa kwasababu pamoja na kuepusha madhara katika makazi ya watu pia inatoa ajira kwa vijana.

Sio wafanyabiashara wote wanaouza mafuta kwa njia holela wanapenda kufanya hivyo, wengine wanashindwa kufungua vituo rasmi kwasababu ya kukosa uwezo wa kufungua vituo hivyo.

Mpango huo wa REA wa kuwadhamini wananchi utatoa fursa kwa wale waliokuwa na mitaji midogo kujiongezea na kufungua vituo rasmi vya kuuzia nishati hiyo.


Vijiji vingi nchini vinakosa huduma ya vituo rasmi vya kuuzia mafuta na huduma pekee wanayopata ni kwa njia ya kuuziwa kwenye chupa.

Ukiangalia vijana wengi wamejiajiri katika kazi ya udereva wa bodaboda na bajaji na hutegemea nishati hiyo kutoa huduma kwa wateja.

Wakisogezewa huduma salama kwenye maeneo yao itawakomboa wengi na pia kuwaepushia vyombo vyao kupata madhara kutokana na kuwa na njia isiyo salama ya kuuziwa mafuta.

Ni matumaini yetu kuwa wananchi watachangamkia fursa hiyo ambayo pia itasaidia kuongeza ajira kwa vijana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Jenifer Gilla

# La uoni hafifu wazazi pia wanapaswa kulaumiwa

**UTAFITI** wa hivi karibu unaofanywa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) na Chuo Kikuu cha Western Applied Sciences cha Norway, umegundua kuwa asilimia kubwa ya wasiojua kusoma wala kuandika wana shida ya uoni hafifu.

Ukifanyika mwaka 2020 katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, unabini kuwa takribani asilimia 60 ya wanafunzi ambao hawajui kusoma na kuandika wana changamoto ya kutoona kikamilifu.

Utafiti huo unaeleza kuwa walimu hawana ujuzi wa kuwawezesha kubaini changamoto hizo, hivyo hushindwa kuwapatia watoto hao afua (njia) wanazostahiki ili wamudu masomo yao, hali inayosababisha kumaliza darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika.

Mkurugenzi Mkuu wa TET, Aneth Komba, akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam, anasema kuwa hali hiyo inachangia baadhi ya wanafunzi kumaliza darasa la saba hawafahamu kusoma, kuandika majina yao, wala kuhesabu.

Anasema, kutokana na matokeo hayo serikali imetenga Shilingi milioni 82.64 kuandaa moduli za kuwafundisha walimu ili waongeze umahiri wa kuwabaini wanafunzi wenye changamoto zinazowarudisha nyuma wakati wa kujifunza katika ngazi ya elimu ya msingi hadi sekondari.

Ukiacha changamoto ya umahiri waliokuwa nayo walimu, wazazi na walezi kuna jambo la kujifunza kufuatia taarifa hii ya utafiti kwa kuwa hata wao wana nafasi kubwa ya kuchangia tatizo hili kutokea.

Wazazi na walezi, wafahamu kuwa zipo changamoto nyingi zinazomrudisha nyuma mtoto katika kujifunza si shuleni tu hata nyumbani, ikiwamo kukoseshwa raha na wanafunzi wenzie na hata kutengwa na kunyanyapaliwa kutokana na kasoro za maumbile walizo nazo.

**Mtoto akiwa huru kumwambia chochote hata kama atarudi usiku atahakikisha anasubiri ili aseme jambo lake.**

Lakini, mtoto anashindwa kuzitolea taarifa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutokuwa na mazingira rafiki kati yake na mzazi, mlezi au mwalimu hasa ukali uliopitiliza hivyo anaamua kuvumilia huku akirudi nyuma kimasomo.

Kuna haja ya wazazi na walezi kuongeza ukaribu, urafiki na upendo na watoto wao ili wawe huru kuwaambia pale wanapopitia changamoto au matatizo mbalimbali.

Mtoto akiwa huru kumwambia chochote hata kama atarudi usiku atahakikisha anasubiri ili aseme jambo lake.

Haiwezekani mzazi au mlezi unalea mtoto huyo tangu akiwa mdogo hadi anamaliza darasa la saba unashindwa kutambua kama anachangamoto ya uoni hafifu au kusikia.

Vilevile wazazi na walezi ni wakati wa kutenga muda wa kucheza na kushirikiana na watoto wenu ili kutambua matatizo yao na wanayoyapitia, itasaidia kwa wale wenye watoto wasioweza kujieleza kwa kuwa utaona kwa vitendo.

Suala la kumsaidia mtoto linahusisha pia kugundua changamoto zinazomkabili katika kujifunza na kuzitafutia ufumbuzi ni jukumu la mzazi na mwalimu.

Kwa maana hiyo, ikiwa mzazi umetambua mtoto anachangamoto ya uoni utakuwa umemsaidia mwalimu kulifahamu tatizo na namna gani ya kumsaidia mtoto huyo darasani.

Wazazi wengi wana dhana kuwa suala la elimu ni jukumu la mwalimu jambalo si wakati ni la ukweli kwa sababu mtoto hasomi shuleni tu hata nyumbani ndiyo maana walimu wanawapa kazi za kufanya nyumbani ili kumpa nafasi mzazi kujua uwezo wa mtoto wake na kumsaidia.

Ni rahisi kumgundua mtoto mwenye uoni hafifu kupitia mwandiko wake na hata jinsi anavyotazama vitu vinavyomzunguka jambo linalohitaji wazazi na walezi kuongeza ukaribu kwa watoto wao ili kulibaini.

Ni wakati wa wazazi na walezi kuamka na kubeba jukumu hili muhimu la kumsaidia mtoto kupambana na changamoto zinazomrudisha nyuma kimasomo ili kutokomeza tatizo la watoto kumaliza darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika.

# Wadau nchini wasisitiza mabadiliko Sheria ya Habari

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa habari nchini wamesema wanapigania mabadiliko ya Sheria ya Habari kwa kuwa ni sehemu muhimu katika maendeleo ya taifa.

Wakizungumza mwishoni mwa wiki kwenye kipindi cha Kipima Joto kinachorushwa na kituo cha Televisheni cha ITV, Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN), Salome Kitomari, alisema vyombo vya habari vinaisaidia serikali kuona na kuchukua hatua na uwapo wa sheria zinazotekelezeka kunaweza kusaidia tasnia hiyo kustawi na kuwa msaada mkubwa kwa serikali.

"Tunaona umuhimu wa kufanya mabadiliko katika sheria hii kwa sababu habari ni maendeleo, lakini habari inaisaidia serikali kufanya uamuzi, inaisaidia serikali kuona mambo ambayo wakati mwingine inaweza isiyaone.

"Kupitia kalamu ya mwandishi, yanaibuliwa mambo ambayo yanaisaidia serikali kuchukua hatua mbalimbali. Kwa hiyo, habari ni kwa ajili ya maendeleo yetu sote," alisema mwenyekiti huyo.

Salome ambaye ni mhariri wa habari wa gazeti la hili, alisema Sheria ya Habari ya Mwaka 2016, imeunda vyombo vingi vinavyosimamia kazi moja ya tasnia ya habari na kwamba hakuna sababu ya kufanya hivyo.

"Tena waziri amepewa mamlaka ya kuteua wajumbe, kwa mfano Bodi ya Ithibati watateuliwa na waziri, sasa uhuru wa hii bodi upo wapi ikiwa waziri ndiyo mwenye mamlaka ya kuteua hawa watu?" Alihoji.

Pia alisema wadau wa habari wamependekeza moja ya mabadiliko muhimu ni kosa la kitaaluma litatuliwe kitaaluma na sio vinginevyo na kama kuna makosa mengine yafuate sheria za nchi.

"Sisi kama wana taaluma, tunapendekeza kosa la kitaaluma litatuliwe kitaaluma, sheria imeishatutambua kama wanataaluma basi hata mambo haya yaende kitaaluma. Hakuna sababu hili suala kuwa jinai, bali lishughulikiwe katika taratibu nyingine," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Deodatus Balile, alisema habari ni haki ya msingi kwa wananchi na nia ya kudai maboresho ya sheria hiyo ni kuwezesha haki nyingine ya msingi kupatikana.

"Baada ya uhai, haki ya msingi inayofuata kwa mtu ni habari. Mwananchi akiwa anakula analala bila kupata taarifa, hatoweza kuendelea na wala kufahamu chochote wala kuendeleza nchi yake. Kwa matokeo hayo, anaweza kuishi kama yupo kwenye mbuga ya wanyama.

"Hivyo tunapodai haki sio kwa ajili yetu bali ni kutafuta haki ya kuwezesha haki nyingine kupatikana kwa faida ya wananchi na taifa letu," alisisitiza.

Raymond Kanegene, ofisa uchechemuzi kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), alisema taarifa ni kitu cha msingi katika jamii na ndiyo maana dunia imeweka Ibara ya 19.

Haki za Binadamu Ibara ya 19 inaeleza kuwa kila mtu ana haki ya uhuru wa kutoa maoni na kujieleza, haki hii inajumuisha uhuru wa kuwa na maoni bila kuingiliwa na kutafuta, kupokea na kutoa habari na mawazo kupitia chombo chochote cha habari bila kujali mipaka.

Pia kuna Mkataba wa Haki za Binadamu 1981, kuanzia hatua ya kimataifa na hadi nchini mwetu katika Katiba yetu ya 1977 Ibara ya 18 inazungumzia mtu kupata habari, kutafuta habari na kusambaza.

"Kama wadau wa haki za binadamu, tunaona ipo haja ya kuangalia baadhi ya hivyo vifungu kwa kufanyiwa marekebisho, kwani wananchi wengi wanatumia vyombo vya habari kufikisha malalamiko. Kufanya hivyo kunaongeza uwajibikaji," alisema.

# Waratibu watakiwa kujiweka kando fedha za sensa

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella, amewaonya waratibu wa Sensa ya Watu na Makazi na kuwataka kujiweka kando na fedha za malipo kwa ajili ya makarani wa sensa na wasimamizi zilizotolewa na serikali.

Shigella alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na watendaji wa serikali katika Halmashauri ya Bukombe na Chato.

Shigella alisema waratibu hao wakijaribu 'kudokoa' fedha hizo zitawaunguza, wahakikishe zinatumika katika malipo ya watu waliokusudiwa na sio vinginevyo.

Alisema fedha hizo zilizotolewa kwa ajili ya malipo ya posho za makarani na wasimamizi wa sensa ni za moto kama fedha za UVIKO- 19, zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alisema kama wapo baadhi ya waratibu wasio waadilifu wenye mawazo ya kuzitumia fedha hizo na kuanza kuwazungusha malipo makarani pamoja na wasimamizi wasithubutu kufanya hivyo.

Aliwataka madiwani katika halmashauri za mkoa huo, kuhamasisha wananchi kwenye maeneo yao ili watoe ushirikiano kwa makarani wa sensa ifikapo Agosti 23, mwaka huu.

Wakati huo huo, Shigella aliwataka watendaji wa serikali kufanya kazi kwa kutanguliza mbele maslahi ya taifa pamoja na uzalendo kwenye usimamiaji fedha za miradi ya maendeleo.

Alitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti wakati akiwa kwenye ziara ya kujitambulisha na kuzungumza na watendaji, madiwani, kutoka halmashauri za wilaya za Geita, Bukombe pamoja na Mbogwe mkoani humo.

Shigella alisema ili kufanikiwa katika kusimamia fedha za miradi ya maendeleo na kukuza uchumi watendaji hao wanatakiwa kutanguliza maslahi ya taifa na uzalendo katika utendaji kazi wao huku akisisitiza ushirikiano.

Mkuu huyo wa mkoa alisema kuwa kufanya kazi bila ushirikiano na kutengeneza makundi ya kisiasa ni ushamba na hivyo kuwataka kubadilika watumishi na watendaji wenye mawazo hiyo.

"Ndugu zangu ili kufanikiwa kukuza uchumi wa wananchi wa Geita watendaji, watumishi wa halmashauri hamna budi kufanya kazi kwa kutanguliza maslahi ya taifa kwanza pamoja na uzalendo," alisema Shigella.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Prof. Godies Kahyarara, alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ana dhamira ya dhati ya kuwatumikia Watanzania na kuhakikisha uchumi wa unakua.

Prof. Kahyarara alisema kuwa kipindi cha awamu ya sita makusanyo ya kodi ya serikali yameongezeka kwa mwezi kutoka Sh. trilioni 1.3 hadi kufikia Sh. trilioni 1.9.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**IMEDURIWA - OMBI LA KUONYESHA NIA: KUBUNI NA KUTEKELEZA MIRADI YA UWEKEZAJI WA KIJAMII KWA MAKABILA YALIYO PEMBEZONI YANAYOJITAMBUA KAMA WAZAWA ASILIA. KUMBUKUMBU NAMBA. 10007446**

EACOP Ltd, Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi, inaalika taasisi (kampuni au AZAKI) zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kubuni na kutekeleza miradi ya uwekezaji wa kijamii kwa makabila yaliyo pembezoni yanayojitambua kama wazawa asilia yanayoguswa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) unatafuta huduma kutoka kwa shirika lenye uzoefu wa kutosha (Kampuni au AZAKI zinaweza kuitikia ombi la kuonyesha nia) ili kubuni na kutekeleza mipango ya uwekezaji wa kijamii na kujenga uwezo kwa jamii za makabila takribani thelathini (30) yaliyo Pembezoni yanayojitambua kama wazawa asilia yanayoguswa na Mradi wa EACOP
Jamii hizi ziko katika mikoa ya Tabora, Manyara, Dodoma na Tanga.

Muundo wa programu utazingatia msaada kwa shughuli za kitamaduni (wafugaji au wawindaji) wa makundi haya ikijumuisha lakini sio tu usimamizi wa ardhi, afya ya mifugo na usimamizi, mahitaji maalum ya wanawake na inapaswa kuundwa kutumia mfumo wa pamoja unaozingatia mahitaji ya uhifadhi na uendelevu.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa uzoefu katika kubuni na kutekeleza miradi ya uwekezaji wa kijamii kwa makabila yaliyo pembezoni yanayojitambua kama wazawa asilia.
- Uthibitisho wa usajili na leseni ya sasa ya biashara kwa makampuni au usajili wa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI kwa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI).
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Ombi la usajili kwenye hifadhi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) na mrejesho wa wakat wa kuwasilisha nia unashauriwa sana kukusanywa.
- Kuzingatia kanuni za ushirikishaji wa wazawa za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya wazawa.
- Ubia kati ya makampuni/mashirika ya kitaifa na kimataifa unaruhusiwa.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi, uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usizidi **20Mb**) saa au kabla ya saa tisa kamili saa za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **24 August 2022.** Kichwa cha barua pepe kiwe **KUMBUKUMBU NAMBA. 10007446.**

Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi (kampuni au AZAKI) zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

Taarifa zote za kuonyesha nia zinapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216992202

# Mpango aipongeza CRDB kwa kukusanya bil.1/- kusaidia jamii

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa pongezi kwa mbio za hisani za kimataifa zinazoandaliwa na Benki ya CRDB, maarufu CRDB Bank Marathon, kwa kufikisha lengo la kukusanya Shilingi bilioni moja kwa ajili ya kusaidia jamii.

Dk. Mpango alitoa pongezi hizo jana wakati akikabidhi mfano wa hundi kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Hospitali ya CCBRT muda mfupi baada ya kukamilika kwa mbio hizo ambazo zilishirikisha zaidi ya wakimbiaji 6,200.

Alipongeza uamuzi wa Benki ya CRDB kuendelea kusaidia upasuaji wa watoto wenye magonjwa ya moyo pamoja na wazo jipya la kusaidia upatikanaji wa huduma salama za uzazi kwa kinamama wenye ujauzito hatarishi.

"Afya ya mama na mtoto ni moja ya maeneo yanayopewa kipaumbele kikubwa katika sera ya afya. Ninafarijika kuona mbio hizi zinasaidia kuimarisha eneo hili kwa kufanikisha upatikanaji wa huduma ya matibabu kwa watoto na kinamama," alipongeza.

Dk. Mpango alisema fedha hizo zilizokusanywa, zitasaidia kupunguza makali ya gharama kwa ajili ya upasuaji wa moyo na huduma za uzazi kwa kinamama wenye ujauzito hatarishi, ambazo watu wengi hawawezi kuzimudu pamoja na serikali kutoa ruzuku ya asilimia 80.

Makamu wa Rais alisema serikali inaunga mkono na kufurahishwa na ubunifu wa taasisi za kizalendo kama Benki ya CRDB kusaidia sekta za kijamii kama vile afya, elimu, mazingira na uwezeshaji kwa vijana na wanawake.

Viongozi mbalimbali walifuatana na Makamu wa Rais kushiriki mbio hizo wakiwamo Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Mussa Zungu, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekule na Waziri wa Michezo Zanzibar, Tabia Mwita Maulid.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alibainisha kuwa mbizo za mwaka huu zimevuka lengo la ukusanyaji wa Shilingi bilioni moja, akitoa shukrani kwa kampuni na taasisi zilizojitokeza kushirikiana na benki hiyo pamoja na wakimbiaji waliojitokeza kutoka ndani na nje ya nchi.

"Kati ya fedha zote Sh. bilioni 1.05 zilizopatikana katika msimu huu wa tatu wa CRDB Bank Marathon, Sh. milioni 250 zimeelekezwa JKCI, Sh. milioni 220 zimeenda Hospitali ya CCBRT, huku fedha iliyobaki kuelekezwa kusaidia kampeni ya mazingira ya Pendezesha Tanzania na resi za ngalawa kule Zanzibar kukuza utamaduni," Nsekela alifafanua.

Nsekela aliwashukuru Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohammed Janabi na Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi kwa ushirikiano wao huku akiweka mkazo kuwa kaulimbiu ya benki hiyo isemayo 'Kasi Isambazayo Tabasamu', imefanikiwa kutokana na mchango wao wa dhati.

Katika mbio hizo washiriki takriban 60 waliofanya vizuri, walijishindia zawadi zenye jumla ya Sh. milioni 100. Zawadi hizo zinaifanya CRDB Bank Marathon kuwa mbio zinazolipa zaidi nchini ambapo washindi wa Km 42 kwa wanawake na wanaume waliondoka na kitita cha Sh. milioni 10 kila mmoja.

Akitangaza matokeo ya mbio hizo, Mkurugenzi wa Mawasiliano Benki ya CRDB, Tully Mwambapa, alisema kwa upande wa kilometa 42, Joseph Munywoki, raia wa Kenya ameibuka kinara akitumia muda wa 02:14:56, wakati Shoron Kosgei, raia wa Kenya aliibuka mshindi kwa upande wa wanawake akitumia muda 02:33:56.

## ATCL kwenda Nigeria, Ghana mwakani

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL), linatarajia kuanza kufanya safari za kwenda nchi za Nigeria na Ghana mwakani, ikiwa ni sehemu ya kupanua na kuboresha huduma za shirika hilo.

Pia linatarajia kuanzisha safari za kwenda miji ya Goma na Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), pamoja na kuboresha miruko ya ndege ya ndani kwa baadhi ya mikoa kwenda mara mbili hadi tatu kwa wiki.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea mojawapo wa kampuni ya wakala wa tiketi za ndege (Skylink).

Matindi alisema: "Tunafanya ziara kwa mawakala wa uuzaji wa tiketi zaidi ya 20. Leo tupo Skylink. Tumefanya mazungumzo marefu yaliyohusu maboresho ya ATCL wanayaonaje, tumewaelezea mipango yetu ikiwamo upanuaji wa mtandao wa safari zetu.

Wametueleza matatizo yanayowasibu, sisi tumewaeleza matatizo ya abiria wetu."

Alisema kwa sasa ATCL imejipanga kuboresha huduma za ndege kwa kurejesha safari zilizositishwa awali na kuanzisha safari mpya kikanda na kimataifa. Matindi alisema ATCL imesharudisha safari za ndege nchini Afrika Kusini na China, ambazo zilisitishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Mkurugenzi Mtendaji wa Skylink, Moustafa Khataw, alisema, watashirikiana na ATCL kuhakikisha wanapata wateja wengi pamoja na kukuza biashara, kuinua Tanzania kiuchumi pamoja na kufaidika na biashara za kimataifa.

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

TAARIFA KWA UMMA

Kumebainika kuwa na **vitendo vya utapeli** ambapo wananchi hupigiwa simu na kudanganywa kuitikia wito wa kwenda Dodoma na **kushinikizwa** kutuma pesa mara moja ili kupatiwa tiketi ya haraka kwani ndege zinakaribia kujaa. **Matapeli** hawa husema tiketi itachukuliwa katika ofisi zetu za mauzo zilizopo Uwanja wa Ndege wa **Julius Nyerere Terminal 2.**

Tafadhali jihadharishe na **matapeli** hawa. Ili kuweza kuhakiki taarifa yoyote unayopewa ya malipo ya tiketi za ATCL piga simu yetu ya BURE ya huduma kwa wateja kupitia namba hii **0800 110045.**

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Mawasiliano**
**Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)**

Air Tanzania The Wings of Kilimanjaro

0800 110045 | www.airtanzania.co.tz

16994502

# Wanafunzi wenye ulemavu waaswa kutumia misaada kujiboresha kielimu

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

WANAFUNZI wenye ulemavu katika shule mbalimbali wilayani Muleba mkoani Kagera, wameaswa kutumia misaada wanayopata kutoka kwa jamii, wadau wa elimu na serikali kuboresha kiwango chao cha elimu ili kutowavunja moyo wanaowasaidia.

Ushauri huo ulitolewa na Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Ziwa, Ladslaus Baraka, wakati akikabidhi msaada wa vitanda 80 na magodoro 160 wenye thamani ya Sh. milioni 27.6 vilivyotolewa na benki hiyo kwa watoto wenye ulemavu wanaosoma Shule ya Msingi Kaigara wilayani Muleba yenye kitengo cha watoto wenye mahitaji maalumu.

Alisema kuwa kupanda kwa ufaulu wa watoto wenye ulemavu kutawapa moyo wanaotoa misaada kuendelea kuwasaidia.

"Msome kwa bidii, tunataka wanafunzi wote wa Kaigara watakaonufaika na misaada hii, tuone ufaulu wenu ukiongezeka kwa sababu mazingira yameboreshwa, serikali imewajengea mabweni na inatoa chakula, NMB imeleta vitanda na magodoro, sasa sijui mshindwe kufaulu kwa sababu gani," alisema Baraka.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Justus Magongo, aliwataka wazazi na walezi wenye watoto wenye ulemavu kuacha tabia ya kuwaficha majumbani kwa kupeleka shule wapate elimu na serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu wanaendelea kuboresha mazingira yao ya kusomea, ikiwamo ujenzi wa shule na miundombinu rafiki.

"Uwapo wa kituo hiki sio kwa bahati mbaya ni kwa sababu serikali inatambua uhai na ustawi wa kila mtu, kumekuwapo tabia ya baadhi ya wazazi, akishajaliwa zawadi ya mtoto ambaye ana mahitaji maalumu, asilimia kubwa wamekuwa wakiwaficha watoto hawa ndani, kwa hiyo serikali kwa kugundua hilo ikaweka sera na miongozo ya kuhakikisha watoto hawa wanapata haki yao ya elimu ya kuishi na kuwajali pia," alisema.

Aliwataka viongozi, watendaji na jamii nzima kwa ujumla kuwa mabalozi na popote ambapo wanajua kuna watoto wenye mahitaji maalumu na wanafichwa ndani, wanapaswa kuhakikisha wamewabaini na wanasajiliwa katika vituo na shule zilizopo ili wapate elimu kwa manufaa yao ya baadaye.

Ofisa Elimu Maalumu wa Wilaya ya Muleba, Neema Rufurano, alisema wilaya hiyo ina watoto 420 wanaosoma katika shule zenye kitengo cha elimu maalumu na elimu jumuishi na kuiomba serikali kuwaongezea idadi ya walimu wenye uwezo wa kufundisha watoto hao ili kukidhi mahitaji yaliyoko.

"Tunaishukuru serikali kwa kuendelea kuwahudumia watoto hawa, inaleta walimu pamoja na huduma nyingine mfano inatoa pesa ya chakula kila mwezi na watoto hawa wote wanasoma bure bila mzazi kuchangia kitu chochote, lakini bado tunayo matatizo mengi ikiwamo ya uchache wa walimu wa elimu maalumu, ingawa mwaka huu tumepatiwa walimu wanane, lakini hawatoshelezi idadi ya watoto tulionao," alisema Rufurano.

# TAKUKURU yabaini mianya upotevu mapato halmashauri

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani hapo imebaini mianya mbalimbali ya upotevu wa mapato katika baadhi ya halmashauri na matumizi ya fedha mbichi kwa visingizio vya changamoto za kimtandao.

Taasisi hiyo pia imefanya uchambuzi katika sekta ya madini, ujenzi, uvuvi na mapato yatokanayo na makusanyo ya POS na kubaini kasoro kubwa za mapato hayo kukatiwa stakabadhi mara mbili na ucheleweshwaji wa kupelekwa benki.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Mzalendo Widege, wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari ya namna walivyotekeleza majukumu ya uzuiaji wa vitendo vya rushwa, uchunguzi na elimu kwa umma, kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2022.

"Kwenye upande wa makusanyo kuna tatizo la baadhi ya watendaji kutumia fedha mbichi kwa visingizio vya matatizo ya mtandao au umbali wa ofisi za halmashauri," alisema.

Widege alisema katika kipindi hicho taasisi imechukua hatua kadhaa katika kukabiliana na changamoto hiyo ikiwamo kuendesha warsha zilizolenga kuziba mianya ya rushwa na upotevu wa mapato hususani kwenye maeneo ya sekta ya madini na mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji.

Pia kwa mujibu wa TAKUKURU, katika kipindi hicho wamepokea malalamiko 70 ya taarifa za rushwa na zisizo za rushwa kwenye maeneo ya ardhi, serikali za mitaa, mahakama, elimu, polisi, afya na sekta binafsi na uchunguzi unaendelea.

"Shabaha iliyoko katika Julai hadi Septemba mwaka huu ni kufanya ukaguzi wa miradi, chambuzi za mifumo, warsha na wadau kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo ili kuweka maazimio ya namna bora ya juziba mianya ya ufujaji iliyobainika," alisema Widege.




Msimamizi wa ufungaji wa mgodi wa Barrick Buzwagi, Michael Wilson, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa kipindi kinachohusu sekta ya madini maarufu 'Thamani ya Madini' mjini Shinyanga mwishoni mwa wiki. (Kushoto) ni Kaimu Meneja Uhusiano na Mazingira katika mgodi wa Bulyanhulu, Zuwena Senkondo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto wanaoishi mazingira magumu wapewa mwelekeo

**Na Romana Mallya**

WATOTO wanaoishi kwenye vituo vya kulea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu wamepewa changamoto ya kubadilisha maisha yao kuwa ni kutumia vizuri fursa ya elimu wanayopata.

Changamoto hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki baada ya Shirika lisilo la kiserikali TAWI Development kwa kushirikiana na mfadhili kutoka Marekani kupitia Taasisi ya LIFE IS US.Inc, walipotembelea vituo viwili vya watoto yatima vilivyoko Chanika, jijini Dar es Salaam na watu wenye ulemavu katika Hospitali ya CCBRT na kuwakabidhi misaada mbalimbali.

TAWI ni shirika linalojiendesha kwa kutotengeneza faida Tanzania lenye lengo la kuinua makundi maalum kwenye jamii kama wanawake, watoto, vijana na wenye ulemavu ambalo lilitoa misaada kwa Kituo cha Kind Heart Africa chenye watoto 72, Msongola Orphanage Trust kinachohudumia watoto 50 na viti mwendo 13 kwa Hospitali ya CCBRT.

Akizungumza baada ya kukabidhi misaada hiyo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10, Mkurugenzi Mtendaji na Mwanzilishi wa TAWI, Naswibu Idrisa, alisema shirika lao litaendelea kutoa misaada ya kielimu.

Idrisa aliwaambia watoto kuwa pamoja na misaada hiyo nguvu ya kubadilisha maisha yao na kufikia ndoto walizonazo zipo mikononi mwao wahakikishe wanasoma kwa bidii.

"Tutaendelea kuwawezesha muwe na maisha yatakayowasaidia kwenye elimu, lakini na nyinyi mna jukumu la kuhakikisha mnafikia ndoto mlizonazo msome kwa bidii, ninatoa rai kwa Watanzania tuwe na utamaduni wa kusaidia makundi haya," alisema.

Mwanzilishi Mwenza wa Taasisi ya TAWI, Sajida Johnson, alisema hakuna msaada mkubwa kwa watoto hao kama kusoma kwa bidii na baadaye kujitegemea.

Alisema wamekabidhi viti mwendo 13 kwa watoto wenye ulemavu katika Hospitali ya CCBRT na kutoa msaada unaojumuisha chakula, vifaa vya kujifunzia, vifaa vya kufanyia usafi, vyakula mbalimbali kwa watoto wa vituo hivyo viwili.

"Tunafahamu Tanzania ina watu wenye ulemavu zaidi ya milioni tatu sawa na asilimia tisa ya idadi ya Watanzania. Tunajua umuhimu wa makundi yote yenye mahitaji maalum, lakini kwa kuanzia tumeona tuanze na watoto hawa," alisema.

Katibu wa Kituo cha Kind Heart, Teddy Joseph, alitaja matatizo wanayokutana nayo ni kitendo cha wafadhili kulipishwa kodi huko nyuma na baadhi kuondoka na kuwafanya kuishi na watoto kwa kuomba kwenye makanisa, misikitini na jamii.

"Mungu awabariki sana leo mmegusa eneo ambalo tulikuwa na changamoto mpaka mmefika hapa ni Mungu amewaelekeza kwa sababu mmeacha vituo vingapi huko mpaka mkachagua Kind Heart.

"Kwa mwezi tunatumia umeme wa Sh. 500,000 kwa sababu tunapandisha maji kwenye kisima, kwa wiki watoto wetu wanatumia Sh. 65,000 kama nauli ya kuwapeleka shule wanazosoma, tunashukuru hakuna aliyeacha kwenda shule kwa sababu ya kukosa nauli, tunalipa vifaa mbalimbali shuleni vinavyozidi ada ambayo serikali imeiondoa," alisema.

Naye Mratibu wa Kujitolea Kituo cha Watoto cha Msongola Orphanage Trust, Mchungaji Zakharia Maloba, alisema wana watoto wanaosoma kuanzia shule za awali, msingi na sekondari na katika matokeo ya kidato cha sita ya mwaka huu mtoto Hillary Khamis aliyepokewa kituoni hapo mwaka 2009 akiwa na umri wa miaka minane, amefaulu kwa kupata daraja la pili lenye alama 2.12.

Rais wa LIFE IS US.Inc, Tumi Oluyole kutoka Marekani, aliwaomba watoto hao wahakikishe wanatumia vipaji walivyonavyo ili waanzilishi wa vituo hivyo wajivunie.

"Mwiangalie hii sehemu mjihakikishie mtafanya mambo mazuri ya kujivunia baadaye, binafsi ni mwalimu na niwasimulie kidogo nilikotoka, huko nyuma nilikuwa sina sehemu ya kulala, sikuwa na kitu, hakuna anayekwambia kuwa wa kwanza kwa kila kitu, kikubwa ni kujituma na kusoma kwa bidii," aliwasihi.

# Mawakala watakiwa kukagua ujenzi barabara kujiridhisha

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

KAIMU Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru mwaka 2022, Emmanuel Chacha, ameuagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), kufanya ukaguzi wa barabara zinazojengwa na makandarasi wanaopewa zabuni kuzijenga kabla hazijakabidhiwa serikalini ili kujiridhisha kama zina ubora.

Alitoa agizo hilo juzi baada ya kukagua na kuweka jiwe la msingi ujenzi wa daraja la Minyinga na barabara ya Utaho-Makiungu, wilayani Ikungi mkoani Singida.

Alisema barabara na madaraja baadhi zinajengwa chini ya kiwango na makandarasi na kuzikibidhi serikalini kwasababu zinapojengwa TANROADS na TARURA hawafanyi ukaguzi kujua kama zimejengwa kwa ubora unaotakiwa.

"Huwezi kukabidhi barabara hata kama ni ya changarawe kabla wewe TANROADS au TARURA hujaipima, pia huwezi kujenga jengo la serikali bila kufanya 'sampling' ya tofali, nondo n.k," alisema.

Awali, Meneja wa TARURA Wilaya ya Ikungi, Mhandisi Ally Mimbi, alisema daraja hilo lililojengwa kwa Sh. milioni 112.1 wakati wa masika lilikuwa linashindwa kupitika na kukata mawasiliano kati ya wananchi wa Jimbo la Singida Mashariki na Singida Magharibi.

Mwenge huo ulizindua kikundi cha Vijana na Maendeleo Ikungi, ambacho kimewezeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kwa ajili ya kuwasaidia kujikwamua na umaskini.

Chacha aliwataka vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kujiunga katika makundi ili waweze kupata mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri.

Mwenge huo pia ulizindua mradi wa maji ya bomba wa Rafiki-Ikungi utakaohudumia kata mbili za Unyahati na Ikungi ambao umejengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 548.7 ikiwa ni sehemu ya fedha za UVIKO-19.

Chacha alisema serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji na kuagiza vyanzo vya maji vinatunzwa ili visiharibiwe na kusababisha kero ya wananchi.

Naye Kaimu Meneja Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Ikungi, Mhandisi Michael Ndunguru, alisema mradi huo umelenga kuwahudumia wakazi 7,500 wa eneo la makao makuu ya Wilaya ya Ikungi linalojumuisha vijiji vya Ikungi na Muungano.

Ndunguru alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kupunguza maambukizi ya magonjwa yatokanayo na ukosefu wa majisafi na salama na kusaidia wananchi kufanya shughuli za kiuchumi na kuondokana na kero ya kutembea umbali mrefu kutafuta maji.



Ofisa wa Idara ya Mapokezi wa Kampuni ya Alliance One, Sadiki Rajabu, akifafanua jambo kwa wakulima wa zao la tumbaku kutoka mikoa ya Kigoma na Tabora walipofanya ziara kwenye kiwanda hicho kilichoko Kingolwira mkoani Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanaharakati apendekeza usawa uteuzi wa viongozi

**Na Yasmine Protace**

MCHAMBUZI wa masuala ya siasa na mtafiti, Deus Kibamba, ameshauri usawa wa kijinsia uzingatiwe katika uteuzi wa viongozi mbalimbali.

"Tunataka katika nafasi za uteuzi zinazofanywa na idara zozote, lazima usawa wa kijinsia uzingatiwe," alisema.

Kibamba akichangia mada kwenye mjadala ulioandaliwa na TGNP Mtandao, kuhusu hali ilivyo kwa wanawake katika nafasi za uteuzi, alisema mamlaka zinazofanya uteuzi ziwe zinazingatia usawa wa kijinsia.

Alisema katika nafasi za kuchaguliwa kuna maeneo wanazingatia jinsia, uwapo wa mwanamke na mwanaume.

Alipendekeza Katiba iandikwe ambayo itasema uwapo wa usawa katika uteuzi na kama haitazingatiwa hatua zichukuliwe kwa wahusika.

"Mamlaka za uteuzi ziweke vigezo katika uteuzi, kuwe na idadi katika ubunge wa kuteuliwa ili kuwapo na usawa wa kijinsia," alisema.

Alisema kukiwa na idadi inayojulikana katika uteuzi kutasaidia kuwapo na usawa.

Alisema katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania idadi ya wanawake asilimia 39, viti maalumu asilimia tisa, madiwani wakuchaguliwa Tanzania asilimia saba na wanawake serikali za mitaa asilimia 2.6.

"Inatakiwa usawa wa kijinsia ufikiwe kwa kupambana na mfumo dume," alisema.

Alisema kuwa TGNP na WLDAF wameanzisha mradi wa usawa wa kijinsia kwa kutumia sheria.

Alisema hoja yake sheria iwepo na kiwango cha uteuzi katika madaraka ya rais kuteua.

Pia utaratibu ufuatwe kila uteuzi na chombo kifuate sheria.

**"Mamlaka za uteuzi ziweke vigezo katika uteuzi, kuwe na idadi katika ubunge wa kuteuliwa ili kuwapo na usawa wa kijinsia," alisema.**

# Makarani sensa wakumbushwa uzalendo

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Murshid Ngeze, ameelekeza makarani wa Sensa ya Watu na Makazi kuwa wazalendo wakati wanapotimiza majukumu yao ili serikali iweze kupata takwimu sahihi.

Ngeze alitoa wito huo juzi alipotembelea na kukagua kituo cha Vikindu cha kutoa mafunzo kwa makarani watakaoshiriki kuchukua taarifa wakati wa sensa Agosti 23, mwaka huu.

Akiwa katika kituo hicho, aliwasisitiza makarani hao kutumia lugha nzuri wanapofika kuchukua taarifa kwa mwananchi.

"Huko mwendako kutekeleza majukumu yenu hakikisheni kuwa mnatunza vizuri vishikwambi (tablets) na vitendea kazi vingine mtakavyopewa kwa ajili ya kujaza taarifa," alikumbusha.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Hadija Nasri, alimshukuru Mwenyekiti huyo kwa kutembelea na kukagua shughuli hiyo katika Wilaya ya Mkuranga na kumwahidi kuwa watafanya vizuri katika sensa kutokana na imani waliyo nayo kwa makarani wao.

Kwa upande wao makarani na wasimamizi wa sensa Wilaya ya Mkuranga, wameahidi kusimamia maudhui ya sensa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizoko.

Yahaya Maramba, mmoja wa makarani hao alisema watazingatia mafunzo waliyopatiwa na kutekeleza majukumu yao kama walivyoelekezwa.

Makarani na wasimamizi hao waliahidi kutunza siri za kila mwananchi watakayemfikia na kuhoji taarifa zake.

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 16, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

## Misitu ilivyo na umuhimu wa kipekee uwepo wa maji



Ukurasa 12

## Serikali inavyomimina upya sekondari kata na wasichana



Ukurasa 13

TEKNOLOJIA

NA ASHTON BALAIGWA, MBEYA

### 'VIFURUSHI' UGUNDUZI KILIMO

# Kuna mpunga supa unaotesa kwenye maji ya chumvi, magadi

## ■ Ipo 'Edeni' ya matundapori tiba watu, mifugo

WIZARA ya Kilimo iwekeze kwenye utafiti ili kuleta tija kwenye kilimo ni maelekezo anayotoa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anapozindua Maonyesho ya Wakulima na Wafugaji Nanenane Mbeya.

Mojawapo ya wadau wakubwa wa utafiti wa kilimo ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ambao wanafanya utafiti mbalimbali kupitia vituo vilivyoko karibu nchi nzima, kuibua matokeo kwa ajili ya kuwasambazia wakulima ili waboreshe kilimo na kuongeza tija.

Kazi hizo ni pamoja na kutafiti na kuibua mbegu na teknolojia ya kisasa ambazo zinahimili ukame na magonjwa mbalimbali.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, akizungumza kwenye Nanenane Viwanja vya John Mwakangale, Mbeya, anasema maonyesho hayo yanayofanyika kikanda, TARI imepeleka timu ya watafiti wa mazao mbalimbali kutoa darasa kwa wakulima.

"TARI jukumu letu kubwa ni kugundua au kuainisha teknolojia kuanzia mbegu na ubunifu wa mbinu za kilimo bora kwenye mazao yote ya kilimo yanayolimwa nchini huku tukiweka nguvu zaidi katika mazao ya kimkakati."

Anazungumzia uanzishwaji wa vituo vya umahiri (centers of Excellency) kwenye kila kanda akisema.

"Katika maonyesho hayo yanayofanyika katika kanda nane zikiwamo Morogoro, Mbeya, Dodoma, Shinyanga, Kagera na Singida. Huduma mbegu, TARI imeanzisha vituo mahiri kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakulima. Kuwafunza teknolojia za kisasa pamoja na kuunganisha mnyororo



Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo (kulia), akipata maelezo ya watafiti wa kituo cha TARI Kibaha mkoani Pwani, kuhusu aina mpya ya mbegu ya mahindi kwenye Maonyesho ya Nanenane Mbeya. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

wa thamani vituo ambavyo vinatoa elimu hiyo muda wote na sio kusubiri Nanenane."

Anaongeza kuwa katika vituo hivyo, mkulima muda wote atakutana na wataalamu kwenye vituo hivyo kuhudumia wakulima kuhusu mbegu bora, kupima udongo, matumizi ya mbolea na kuwaelekeza dawa za kutibu udongo uliochoka.

Anaongeza kuwa uanzishwaji wa vituo hivyo mahiri umelenga kuwasogezea huduma karibu zaidi wakulima kwa ajili ya kujifunza teknolojia zilizogunduliwa na watafiti kwenye mazao yote ili kuongeza fursa ya kuongezea tija kwa kutumia mbegu na teknolojia za kisasa zaidi ambazo zimegundulika.

VIFURUSHI UGUNDUZI

Katika maonyesho hayo, Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Dakawa kilichoko wilayani Mvomero Morogoro ambacho kinafanya utafiti wa mpunga, Dk. Jorome Mghase, anazungumzia mafanikio ya kilimo cha mpunga.

Anaelea kuwa, wamefika Nanenane na teknolojia ya mbegu mpya za mpunga, ambazo ni mkombozi kwa wakulima wa zao hilo na kwamba walioacha kilimo hicho kutokana na mashamba yao kuongezeka chumvi, magadi na changamoto ya wadudu pamoja na mabadiliko ya tabianchi watarejea mashambani.

Anawahakikishia kwamba, hivi sasa watarudi katika kilimo hicho kwa tija na watakifurahia baada ya kugundua mbegu za mpunga za'Sato1, Sato9' ambazo zinahimili ardhi yenye chumvi na magadi wakati, TARI Ric1, TARI Ric2 na Komboka zina uwezo wa kukabiliwa na mabadiliko ya tabianchi pamoja na wadudu waharibifu.

Anasema teknolojia ya mbegu hizo imefanyiwa majaribio katika maeneo saba yanayolimwa mpunga kwenye ikolojia tofauti na zimeonyesha kuleta tija na kuongeza uzalishaji wa zao mpunga.

MATUNDAPORI TELE

Mkurugenzi wa Kituo cha TARI -Tumbi cha Mkoani Tabora, Dk Emmanuel Mrema, anasema wamefanya utafiti na kubaini kuwepo kwa zaidi ya aina 50 za miti ya matunda pori kwenye misitu ya miombo hapa nchini yenye uwezo wa kuchangia usalama wa chakula endapo Ikolojia yake itaendelezwa.

Anasema, miti hiyo ya matundapori imebainika kuwa na uwezo wa kutoa lishe na tiba ya kumaliza tatizo la udumavu na kutaka wakulima na wananchi kujitokeza

INAENDELEA UK. 14

ELIMU

NA MARY GEOFREY

# Serikali inavyomimina upya sekondari kata na wasichana

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetoa Shilingi bilioni 100.58 kujenga sekondari mpya 214 zitakazojengwa kwenye kata zote, aidha bilioni thelathini zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa sekondari mpya za wasichana kwenye mikoa 10 ikiwa ni shule moja katika kila mkoa Tanzania Bara.

Mradi huo uliopewa jina la Secondary Education Quality Improvement Program - SEQUIP, unazihusu shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita, kazi ikifanyika kwa miaka mitano kadi 2025. Hayo yanabainishwa wakati wa ziara ya Katibu Mkuu CCM, Daniel Chongolo, mkoa wa Kilimanjaro.

Kilimanjaro, inatekelezwa kwenye kata za Mnadani, Kundi na Njiapanda wilaya ya Moshi, Msaranga na Kivisini wilaya ya Mwanga, Mamsera wilaya ya Rombo, Kisima na Ndugu wilaya ya Same na Biriri wilaya ya Siha, Chongolo, anafanya ziara na kutembelea miradi hiyo ya shule. Aidha, katika ziara hiyo inafahamika kuwa utekelezaji wa mradi wa SEQUIP upo kwenye maeneo ya vipaumbele vya serikali yanayogusa elimu ya sekondari ambayo ni ujenzi wa shule mpya za sekondari 1,000.



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo (katikati), akiwa kwenye ziara kutembelea mradi wa ujenzi wa sekondari mkoani Kilimanjaro. **PICHA: MARY GEOFREY**

Sekondari zinazojengwa kwenye kata ambazo hazina maeneo ambayo yenye wanafunzi wengi ukilinganisha na miundombinu iliyopo, wakati sekondari za wasichana ni kwa kila mkoa na kwamba kazi inafanyika kadri fedha zinavyopatikana na kwa sasa wanaendelea na uchambuzi ili kujenga shule za nyongeza 20 kwenye kata zenye msongamano wa wanafunzi.

Gharama ya ujenzi wa sekondari za kata ni milioni 600, kwa kila shule, awamu ya kwanza ikianza na Shilingi milioni 470.

Chongolo,anatembelea baadhi ya shule hizo Kilimanjaro kukagua utekelezaji wa mradi huo na wa ilani ya chama hicho ya mwaka 2020/25 na kukagua miradi mingine ya maendeleo akihimiza ujenzi wa shule ukamilike kwa wakati na zijengwe kwa ubora unaotakiwa.

Katibu Mkuu anaridhishwa na kazi katika baadhi ya shule na kuhimiza wanafunzi kusoma kwa bidii, lakini pia wananchi kutunza majengo hayo ambayo yanajengwa kwa fedha za serikali kwa asilimia 100.

"Ilani imeahidi elimu na ninyi ni mashahidi, Rais Samia Suluhu Hassan na serikali imeshapeleka fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule. Ilani imeahidi na serikali inafanya kazi kubwa katika maeneo hayo na maeneo mengine. "Nipongeze kamati zinazosimamia na kuratibu ujenzi wa shule hizi,tumepita tumeangalia miundombinu na tumeridhika,"anasema Chongolo.

Pamoja na umuhimu wa madarasa pia anataka kuwepo na viwanja vya michezo kwasababu ni sehemu ya elimu na kusisitiza watoto wacheze na wasome kwa mujibu wa ratiba zilizopo.Ujenzi wa shule hizo unajumuisha ofisi ya walimu, vyoo, maabara za sayansi na maktaba.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa TAMISEMI, Nteghenjwa Hosseah, anasema gharama ya ujenzi wa shule za sekondari za wasichana za mikoa ni Sh. bilioni nne ambapo Sh. bilioni tatu zimetolewa ikiwa ni malipo ya awamu ya kwanza ya ujenzi kwa kila shule.

Anasema shule za sekondari za kata zitachukua wanafunzi takribani 400 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na zitachukua wanafunzi wasiopungua 1,000 kwa kila shule.

Anasema, mradi huo wa SEQUIP umelenga kuongeza sekondari, kuweka mazingira salama ya elimu kwa wasichana na kuhakikisha wanafunzi wote wanapata elimu bora ya sekondari na kwamba ufuatiliaji wa fedha hizo wizara imetoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa na wakurugenzi halmashauri zote.

Anataja mojawapo ya maelekezo kuwa halmashauri kuhakikisha kuwa maeneo yaliyoteuliwa kwa ajili ya ujenzi wa shule hizi hayana migogoro ya umiliki wa ardhi, mengine ni halmashauri za majiji na manispaa zenye ufinyu wa maeneo ya ujenzi zinaruhusiwa kujenga ghorofa, pia kuomba kibali cha kutumia kiasi kilichotengwa na mapato ya ndani kukamilisha ujenzi.

"Ilani imeahidi elimu na ninyi ni mashahidi, Rais Samia Suluhu Hassan na serikali imeshapeleka fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule. Ilani imeahidi na serikali inafanya kazi kubwa katika maeneo hayo na maeneo mengine.

Maelekezo mengine ni kazi za ujenzi zinatakiwa kuanza ndani ya wiki mbili baada ya kupokea fedha na mwongozo wa ujenzi na kukamilika ndani ya miezi sita kwa sekondari za kata na mwaka mmoja kwa shule za sekondari za mikoa.

Nteghenjwa anasema, pia kuzingatia taratibu za usimamizi wa mazingira na ushirikishwaji wa jamii husika kabla, wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi kukamilika ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza kama vile ukataji wa miti hovyo, uchafuzi wa mazingira na unyanyasaji wa kijinsia.

Maagizo mengine yalikuwa ni mradi huo unaweza kutekelezwa kwa kutumia utaratibu wa "forceaccount" au Wakandarasi na kuwa gharama za ujenzi kwa kutumia njia yoyote zisizidi fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli husika.

Mradi huo unatekelezwa na TAMISEMI,Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ukilenga kuboresha elimu ya sekondari nchini na unagharamiwa na serikali kwa mkopo wa takribani Shilingi trilion 1.1 mkopo kutoka Benki ya Dunia.

**MATUMAINI WANUFAIKA**

Wanufaika wa mradi huo ambao ni wanafunzi wa mkoa huo, akiwamo Magdalena John, kutoka Kijiji cha Naibi, kata ya Biriri, wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro, anasema kwa wataondokana na adha ya kutembea kilometa 12 kufuata sekondari zilizoko katika kata za Makiwaru na Sanya Juu. Wakazi wa kijiji hicho hawajawahi kuwa na sekondari tangu uhuru lakini sasa watanufaika na mradi huo.

"Tunaamini wanafunzi watasoma kwa utulivu, muda waliokuwa wakitumia kufuata elimu kata za jirani watautumia kusoma na kuongeza ufaulu wao," anasisitiza Magdalena.

Ujenzi wa shule hiyo, unaohusisha madarasa nane, jengo moja la maktaba, matundu 28 ya vyoo, chumba cha TEHAMA, maabara sita za masomo ya sayansi na jengo moja la utawala, upo katika hatua za mwisho za kukamilika.

ELIMU

NA DK FELICIAN B. KILAHAMA

# Misitu ilivyo na umuhimu wa kipekee uwepo wa maji



Misitu inatunza ardhi na kudhibiti mmomonyoko wa udongo. **PICHA: MTANDAO**

NIKIAMINI kwamba wasomaji wa makala hii ni wazima wakimtukuza Mungu ambaye kwa rehema zake ametujalia zawadi ya uhai, lakini tukumbuke kuwa uhai wetu unategemea tunywe maji, tuvute hewa safi, tulime na kufuga kwenye ardhi isiyochafuliwa ili kulinda afya.

Katika makala iliyopita iliangazia misitu na maji hususani jinsi misitu inavyofanikisha mito kutiririsha maji majira yote. Leo, makala hii inatazama umuhimu wa misitu kuhifadhi ardhi na udongo na uhusiano wake na maji ya mvua.

Ardhi, ni rasilimali muhimu kwa maisha ya binadamu na viumbe wengine wapo wanyamapori na mimea, kimsingi bila ardhi hakuna maisha. Mungu aliumba nchi kavu na sehemu kubwa ikafunikwa na maji ambayo ni ardhioevu, aidha, aliweka vitu vingi kwenye nchi kavu ukiwamo udongo ambao ni msingi wa mimea, miti na mazao mbalimbali bila kusahau wanyamapori na wafugwao.

Katika ardhioevu (mazingira yenye maji muda wote) kumesheheni vitu vingi wapo samaki aina mbalimbali, viboko, mamba, mimea na miti kama mikoko.

**KUTUNZA UDONGO**

Misitu ambayo ni miti pamoja na kutumia udongo ili kuota, mizizi kujishikiza na kustawi inahitaji unyevu wa kutosha; inasaidia udongo kuwa katika hali inayofaa. Uoto wa asili na misitu ya aina mbalimbali, ikiwamo ya kitropiki katika sehemu zenye mvua nyingi, joto la kutosha hupatikana zaidi sehemu zenye miinuko na milima katika ukanda wa tropiki.

Tanzania kwa sehemu kubwa ilijaliwa kufunikwa na misitu aina ya 'Miombo' iliyosheheni aina mbalimbali za miti mathalani, mitundu, miminga, mipangapanga, migunga, mikarambati, miyombo zikiwamo aina za miti ya matundapori kama fulu, misada, ndonga, misalu na misasati.

Kadhalika ipo misitu ya Ukanda wa Pwani yenye mikoko inayostawi ndani ya maji ya chumvi au baharini na miti ya matunda kama mikwaju.

Kimsingi, ardhi au udongo vikiwa vimefunikwa na mimea, misitu rasilimali iliyo salama na thamani yake ni kubwa, inaendelea kustawi. Wakati Tanzania inapata uhuru Desemba 9, 1961, sehemu kubwa ya nchi takribani zaidi ya asilimia 80, ilikuwa imefunikwa na misitu.

Sasa ni miaka zaidi ya 60 tangu uhuru, asilimia kubwa ya misiti na uoto wa asili, vimetoweka. Uzoefu unaonyesha kuwa mikoa ya Kanda za Ziwa, Kati, Kaskazini, Mashariki na ukanda wa Pwani kuanzia Mtwara hadi Tanga imeathirika mno.

Mikoa ya magharibi na nyanda za juu kusini hadi Ruvuma pia kasi ya kutoweka misitu inaongezeka. Kukata miti, kufyeka misitu na kuchoma moto mapori na misitu, ni tishio kubwa kwa uhai wa taifa.

Shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwamo kuanzisha makazi, kilimo cha kuhamahama, maeneo ya kuchungia mifugo, matumizi makubwa ya kuni na mkaa vijijini na mijini, kutumia kuni kwa kiwango kikubwa kukaushia tumbaku katika mikoa ambako tumbaku ni zao la biashara, vilevile, kuzitumia kutengeneza chumvi hususani eneo la Uvinza mkoani Kigoma zimeathiri mno misitu.

> Isitoshe zipo baadhi ya shughuli pia zinazotumia kuni mfano, kukausha samaki, pamoja na kuchoma matofali. Changamoto hizo na nyingine nyingi kwa ujumla husababisha misitu kutoweka kwa haraka sana.

Isitoshe zipo baadhi ya shughuli pia sinazotumia kuni mfano, kukausha samaki, pamoja na kuchoma matofali. Changamoto hizo na nyingine nyingi kwa ujumla husababisha misitu kutoweka kwa haraka sana.

Kwa sasa kuna changamoto kubwa ya kutengeneza mkaa katika mikoa ya magharibu na isitoshe wahamiaji wengi kutoka maeneo mengine wamejikita huko wakiwa na mifugo mingi kuvamia mapori ili kulisha wanyama.

Kutokana na hali hiyo, misitu inafyekwa na miti kukatwa kwa matumizi ya mkaa na kuni na kuanzisha makazi mapya na mashamba. Uwezo wa serikali za vijiji, halmashauri za wilaya na hata Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kusimamia misitu ya asili iliyo katika mamlaka yake kisheria, mfano, TFS kusimamia misitu ya serikali kuu iliyohifadhiwa kwa kuzingatia Sheria ya Misitu (Cap 323 RE:2002) ni mdogo; hivyo uharibifu unakuwa mkubwa.

**KITISHO JANGWA**

Mathalani, kituo na kutathimini masuala ya gesi ukaa kilichoko Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Morogoro, mwaka 2017 kilitoa taarifa kuwa uharibifu wa misitu nchini ulikuwa umefikia kiwango cha hekta 469,000 kwa mwaka ikiwa ni ongezeko la hekta 97,000 ukilinganisha na takwimu za Wizara ya Maliasili na Utalii za 2015 zilizoonyesha kasi ya hekta 372,000 ya kutoweka kwa misitu.

Hali hii haipendezi kimazingira na kwa kutilia maanani kwamba kasi ya mabadiliko ya tabianchi nayo ni tishio duniani. Iwapo eneo kubwa la nchi litakuwa limefunikwa na misitu kwa asilimia zaidi ya 50, taifa linakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji ya mvua ya kutosheleza mahitaji ya mwaka mzima kupitia chemichemi, vijito na mito kutiririsha maji muda wote.

UWEPO MAJISAFI

Maji yatakayotiririka kwenye mito yatakuwa safi hayatakuwa na udongo au uchafu kama hali ilivyo sasa. Isitoshe, hata gharama za kuendesha mamlaka za maji zitapungua kwa sababu hazitalazimika kutumia fedha nyingi kuyasafisha ili kuyasambaza.

Kimsingi misitu ni muhimu licha ya kuvuta mawingu ya mvua, pia husaidia kupunguza kasi ya mvua hivyo kuwezesha maji ya mvua kuingia taratibu ardhini. Eneo kubwa likiwa limefunikwa na misitu changamoto ya mmomonyoko wa udongo hasa kwenye vilima na miteremko haitokei kama ilivyo kwenye sehemu zilizo wazi.

Hata upepo mkali ukivuma hauleti athari kubwa, lakini eneo likiwa wazi upepo hupeperusha chembechembe laini za udongo, ambazo ni muhimu kwa ustawi wa mazao na kuupeleka mbali.

Hivyo, husababisha ardhi kuwa kame na kukosa rutuba hivyo kuonekana haifai kwa shughuli za kilimo. Hali ikiwa hivyo, wakulima huvamia maeneo mengine ya misitu na kuendeleza uharibifu na kuweka rehani hatima ya wanyamapori kwa kudhoofisha ikolojia stahiki kwa ujumla.

Kuna uhusiano mkubwa kati ya misitu, maji, mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Bila misitu maji yatapungua kwenye mito na ardhini na bila maji misitu haistawi vizuri na kuathiri pia maisha ya wanyamapori na mimea mbalimbali.

Matokeo hatarishi ni pamoja na shughuli za kilimo, ufugaji pamoja na utalii kuathirika. Hatua zinazochukuliwa na serikali kwa kufanya shughuli za kilimo na ufugaji kuwa za kisasa, iwapo zitatekelezwa kama inavyodhamiriwa, huenda ndani ya kipindi kifupi Tanzania ikarejesha misitu na uoto wa asili katika maeneo kadhaa yaliyokuwa yameharibika.

Inamaanisha kuwa iwapo zaidi ya asilimia 50 ya wakulima na wafugaji watatumia mbinu za kisasa (kilimo na kufugaji kijani), eneo dogo la ardhi litumiwe kuzalisha mazao ya kutosha na bora ya kilimo au mifugo, hakuna sababu ya kufyeka eneo kubwa la misitu. Hata, maeneo yaliyoharibiwa yataweza kuboreshwa na hatimaye kurejea kwenye uhalisia wake wa mwanzo.

Tutaweza kuhifadhi udongo, maji na bioanuwai kwa gharama nafuu na kupata matokeo makubwa kwa faida yetu na jamii zote.

Hivyo, kila jitihada zifanyike kudhibiti kasi ya kutoweka misitu nchini. Inawezekana ni jukumu la watu wote kama jamii, taifa na kimataifa. Katika toleo lijalo makala itafafanua uhusiano wa misitu na sekta ya nishati.

TEKNOLOJIA

# Kuna mpunga supa unaotesa kwenye maji ya chumvi, magadi

INATOKA UK. 11



Mpunga supa unaostawi sehemu zenye magadi na chumvi ni tumaini jipya la wakulima wa mkoa wa Morogoro.**PICHA: MTANDAO**

katika banda la TARI kupata elimu hiyo. Dokta Mrema anasema katika utafiti huo pia, miti hiyo ya matunda pori inatunza mazingira na kuongeza kipato kwa mkulima kwakuwa inauwezo mkubwa wa kuhimili ukame kwa kipindi kirefu ukilinganisha na miti mingine ya asili.

**BYE UDUMAVU**

Anataja baadhi ya miti hiyo ya matundapori ni pamoja na ntonga yenye uwezo wa kusaidia kumaliza tatizo la udumavu na magonjwa yanayotokana na upungufu wa vitamin na viini muhimu kwa ajili ya tiba ya magonjwa ya binadamu na mifugo.

" Hii miti ya matunda pori inaweza kuwa chanzo muhimu sana cha chakula, lishe na madawa na kusaidia kupiga vita utapiamlo na upungufu wa vitamin A na C, amino aside, muhimu na madini kama chuma na zink" anaongeza.

**KUPIMA UDONGO**

Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Mlingano kilichopo mkoani Tanga, Dk Catherine Senkoro, anasema katika maenyesho hayo ya wakulima na wafugaji ya nanenane wakulima watapata nafasi ya kujifunza matumizi ya udongo kulingana na mazao wanayokusudia kulima katika maeneo yao ikiwamo na fursa ya kupimwa kwa udongo.

" Tupo hapa ili kuwasaidia wakulima na kuwashauri kabla ya kuamua kufanya kilimo cha mazao mbalimbali ni vyema wakapima udongo wa shamba. ili kujua na kupata ushauri nini cha kufanya ili wapate tija katika kilimo" anasema Dk. Catherine.

Anaongeza kuwa, wakulima hao watakaofika katika maonyesho hayo na vituo mahiri watajifunza jinsi ya kutumia mazao ya mikunde kunde na fiwi yenye uwezo wa kuchanganywa na mazao mengine kuongeza mboji katika udongo pamoja na kudhibiti magonjwa ya minyoo na magugu.

Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu wa TARI, Dk Joseph Ndunguru,anasema utafiti wote wa teknolojia mpya za mbegu zilizoibuliwa zimeonyesha uwezo mkubwa baada ya kufanyiwa majaribio. Zinaweza kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabianchi, wadudu na ukame .

Dk. Ndunguru anasema:" Kutokana na kuwepo kwa teknolojia hizo za kisasa tayari vijana wameshaanza kuvutiwa kufanya kilimo biashara kitakachochukua muda mfupi kutokana na kuwepo kwa uhakika wa kupata mavuno kwa muda mfupi na kuachana na kutegemea ajira"

Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu anawataka wakulima nchini kutumia Nanenane na vituo umahiri kupata elimu ya kilimo cha kisasa na chenye tija ili waweze kujiongezea kipato.

Akiendelea kuzungumzia utafiti na ugunduzi, Mkurugenzi Mkamiliko, anasema TARI imekuja na teknolojia zote za kilimo zilizogunduliwa na watafiti mahiri kutoka vituo vyake ili kuelimisha jamii na wakulima Halikadhalika, anaongeza kuwa lengo la kupeleka timu ya watafiti katika kanda za maonyesho ni ili wakulima na jamii wapate elimu ya kutosha kuhusu teknolojia hizo zilizogunduliwa.

Mkurugenzi Mkuu anasema, jambo lingine wanalofanya ni uhaulishaji wa teknolojia ambao wanashirikiana na halmashauri mbalimbali za miji na wilaya hasa maofisa ugani pamoja na vyombo vya habari lengo ni kutaka mkulima apate taarifa ili alime kisasa mazao ya chakula na biashara.

Anasema, teknolojia na mbegu hizo zimeonyesha kuwa zina uwezo wa kupambana na magonjwa, ukame wadudu waharibifu pamoja na mabadiliko ya tabianchi na sifa kuu ni kuongeza zaidi uzalishaji.

Fursa nyingine ambazo wakulima watazipata katika vituo hivyo mahiri pia ni kufundishwa jinsi ya kutumia mbinu za vidhibiti magonjwa na wadudu waharibifu katika mashamba yao.

"Lengo la TARI ni kutaka kumbadilisha mkulima kuachana na kilimo cha mazoea ambacho kimepitwa na wakati na badala yake kufanya kulima kisasa kwa kutumia teknolojia bora zaidi zilizoibuliwa na watafiti mahiri".

" Tunataka mkulima anapokuja katika maonyesho na pia anapotembelea vituo mahiri aondokane na mtazamo wa kilimo cha mazoea badala yake atumie hizi teknolojia za kisasa ili aongezea tija " anasema Dk.Mkamilo.

TARI inafanya utafiti na kuboresha uzalishaji wa mazaoya mkakati ambayo ni mahindi, mpunga, pamba, korosho, chai, kahawa, tumbaku, mkonge, michikichi, zabibu, ngano, maharage ya soya, cocoa, mhogo, miwa, mboga, matunda na alizeti.

## WANENAVYO MALENGA

# NYIE VIONGOZI WETU

WASHUHUDIE foleni, ili watutatulie,
Tuwe nao mitaani, vibaka wawaibie,
Pesa zao mfukoni, mafuta wanunulie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Sisi tujichagulie, na viti wavikalie,
Na halafu tusalie, mengi tulalamikie,
Wenyewe tuangalie, keki yetu wajilie,
Hapo matatizo yetu, hatupati utatuzi.

Yale tunayapitia, na wao wayapitie,
Pale tunapoumia, pia wao waumie,
Ndipo watapoanzia, yote washughulikie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Muda wao wa kula, hilo tusilisikie,
Ni kazi bila kulala, hiyo kwao tusikie,
Hii ya kwetu misala, na wao iwafikie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Sisemei huku kwetu, nitaje unisikie?
Hili hili bara letu, hebu tuliangalie,
Hawa viongozi wetu, ili tuwafurahie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Kabla zetu chaguzi, tuliko watufikie,
Hata kama twala ndizi, na wao tuwagawie,
Hata makundi sogozi, humo nao waingie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Ukitoka kijiweni, zao kura wapatie,
Washinde wawe enzini, jaribu uwafikie,
Ni kama madhabahuni, si rahisi ufikie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Hujamchagua wako, ili akutumikie,
Kura zako za mashiko, kitiche akikalie,
Ni kudra kwako, jaribisha umwingie,
Hapo matatizo yetu, hayapati utatuzi.

Afrika tuamke, tusibaki tusinzie,
Viongozi tuwapike, sisi watutumikie,
Nasi nafasi tushike, kazi tusijivunie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

Nyie viongozi wetu, pongezi ziwafikie,
Mnaojali ya kwetu, acha tuwashangilie,
Ziko vema kura zetu, bora tujifagilie,
Hapo matatizo yetu, yatapata utatuzi.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



HABARI DODOMA

# Wizara ya Maji yataja vipaumbele vyake vitano

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Maji imetaja vipaumbele vyake vitano kwa mwaka 2022/23, ikiwamo kuboresha ufanisi katika matumizi ya maji ili kuepusha nchi kuwa na uhaba wa maji.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Maji, Maryprsica Mahundi, alisema rasilimali za maji zilizoko nchini zinakadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka.

"Kwa mwaka wa fedha 2022/23 serikali itaendelea kuwekeza katika utunzaji wa vyanzo vya maji, ujenzi wa miundombinu ya kuongeza upatikanaji wa maji, kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Alisema wamepanga kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea kutekelezwa na serikali.

"Pia kuanza ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa pamoja na kuanza ujenzi wa miradi mipya ya maji katika miji 28," alisema.

"Wizara imejipanga kuhakikisha sekta ya maji inazidi kuboreshwa ili kuondoa kero ya maji kwa wananchi mijini na vijijini," alisema.

Alibainisha kuwa wizara hiyo itahakikisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini inafika zaidi ya asilimia 85 ifikapo 2025, huku wamepanga kutekeleza miradi 1,029 ya maji.

"Wizara imepanga kutekeleza jumla ya miradi 175 yenye kulenga kuboresha upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi waishio mijini na kuongeza kuwa utekelezaji huo ni sehemu ya kufikia asilimia 95 ifikapo 2025," alisema.

Mahundi alisema katika kuhakikisha sekta ya maji inakuwa na wataalamu wa kutosha na wenye weledi wa hali ya juu serikali itaendelea kukiimarisha na kukitumia Chuo cha Maji ili kutoa wataalamu bora.

# Upungufu magari kubeba wagonjwa chanzo vifo

**Na Magdalena Jackson,** SJMC

UPUNGUFU wa magari ya kubeba wagonjwa maeneo ya vijijini umetajwa kuchangia vifo vingi kwa wajawazito na watoto wachanga.

Kutokana na hali hiyo, kupitia Mradi wa M-Mama wa Vodafone Foundation, wamiliki wa usafiri binafsi wanatarajiwa kuingizwa kwenye mfumo ili kusaidia kutatua tatizo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akizungumza wakati wa uwasilishaji wa huduma ya usafiri wa dharura kwa wajawazito, waliojifungua na watoto wachanga inayotekelezwa na mradi huo, alisema kuingiza usafiri binafsi kutasaidia kuwaokoa wajawazito na watoto kupata usafiri wa dharura.

"Serikali itawatambua na kuwachagua wamiliki wa magari katika kila kijiji na kuingia nao mkataba katika halmashauri na kuingizwa katika mfumo wa M-Mama ili kuhusika katika usafirishaji wa wagonjwa wa dharura," alisema.

Alisema mradi huo ulifanyiwa majaribio kwa awamu mbili katika wilaya ya Sengerema na Shinyanga na serikali iliona mfumo huo unafaa kutekelezwa nchi nzima.

Aidha, alibainisha kuwa Mkoa wa Dodoma umefanikiwa kuongeza idadi ya vituo vya afya vinavyotoa huduma ya dharura ya upasuaji kutoka vituo 24 mwaka 2018 hadi 35 mwaka 2021 pamoja na vingine zaidi ya 23 ambavyo vipo katika ujenzi.

"Mkoa wa Dodoma pamoja na kamati zake kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, tumepiga hatua kubwa katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, mwaka 2019 vilikuwa 74, mwaka 2020 (88) na 2021 (68)," alisema.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, alisema asilimia kubwa ya kinamama na watoto wanaofariki ni kwa sababu ya kuchelewa kufika kupata huduma ya matibabu, mpango huo wa usafiri ukichukuliwa kwa umakini utasaidia kutatua tatizo hilo vijijini.

Kwa upande wake, Mwakilishi Kitengo cha Uzazi na Mtoto wa mkoa huo, Dk. Sunday Dominico, alisema moja ya sababu kubwa ya vifo vitokanavyo na uzazi ni mfumo wa rufani kutokutimiza malengo yanayotarajiwa.

Pia, alisema mpango huo wa M-Mama unakwenda kuongeza uwajibikaji na usimamizi kwa kutumia teknolojia ya kuimarisha mfumo wa rufani.

Mkurugenzi wa M-Mama Vodafone Foundation, Dolorosa Dancan, alisema kufikia Novemba mwaka huu mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na sita ya Zanzibar itafikiwa na mfumo huo.



Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Lusako Kilembe (kushoto), akitia saini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Makole jijini Dodoma na Uongozi wa Nyanza Road Works Ltd ambao uliwakilishwa na Jay Patel (kulia) na Vijay Krishine (wa pili kulia), huku mwanasheria wa TARURA mkoani humo, Suzana Senso akishuhudia. **PICHA: IBRAHIM JOSPEH**

# Wamiliki migodi marufuku kununua baruti holela

**Na Magdalena Jackson,** SJMC

OFISI ya Madini Mkoa wa Dodoma imewapiga marufuku wamiliki wa migodi kununua baruti kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi ili kujiepusha na majanga yatakayojitokeza kwa watumiaji.

Aidha, Mkoa wa Dodoma unakabiliwa na uhaba mkubwa wa vilipuzi hivyo ikiwa mahitaji ni tani 400 hadi 800 za baruti kwa mwezi huku zilizoko ni tani 100.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Nchagwa Marwa, alibainisha hayo jana baada ya kukagua kiwanda cha utengenezaji baruti Kilondo, kilichopo mgodi wa Nholi wilayani Bahi.

Alisema kwenye maeneo yasiyo rasmi wanunuzi wa baruti wanakosa elimu ya namna bora ya kutumia hali inayohatarisha maisha yao.

Alisema Mkoa wa Dodoma unauhitaji mkubwa wa baruti na kuwataka wawekezaji kujitokeza kuwekeza ili kuondokana na uhaba wa vilipuzi hivyo vya migodi.

"Licha ya uwapo wa uhaba wa bidhaa hizi mkoani hapo nawataka wamiliki wa migodi kuacha kabisa kununua baruti kwa njia zisizo rasmi na maeneo yasiyokuwa rasmi," alisema.

Kwa upande wake, Meneja wa Mgodi wa Nholi, Kulwa Limbu, alisema kutokana na kuwapo kwa maghala ya baruti yaliyojengwa na wawekezaji kutoka kiwanda cha Kilondo kutasaidia kutatua uhaba wa upatikanaji wa bidhaa hiyo iliyokuwapo tangu mwaka 2020 ya watu kununua kwa njia zisizo bora na salama.

"Wachimbaji kwa sasa hakuna sababu ya kununua baruti za vichochoroni kwa sababu kuna maeneo yaliyoruhusiwa yenye wataalamu ambao watawaelekeza namna ya kusafirisha na kutumia kwa usalama na utaalamu zaidi," alisema.

Kadhalika, aliwataka wachimbaji na wamiliki wa leseni kuachana na vitendo viovu vya kutorosha madini bali wazingatie taratibu ya kujaza fomu za mwalo zinazoonesha taarifa za uzalishaji ili kupunguza utoroshaji huo na kupata fursa ya kupata mikopo.

Naye mtaalamu wa baruti Kilondo, Justine Nzasule, alisema kampuni hiyo inajihusisha na utoaji wa huduma zenye usalama na utaalamu kwa jamii ikiwa ni pamoja na kusaidia serikali kwenye urasimishaji na matumizi salama ya baruti.

Kadhalika, alisema kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa mafunzo ya baruti kutoka vyuoni na kutoa huduma kamili ya vilipuzi na kulipua katika migodi mikubwa na midogo.



# Miche ya kahawa ya kisasa milioni saba kusambazwa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

ZAIDI ya miche ya kisasa ya kahawa 7,000,000 inatarajiwa kusambazwa kwa wakulima katika mikoa mitatu ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayozalisha zao hilo ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo pamoja na kuongeza kipato cha familia.

Pia zaidi ya kaya 24,000 zinatarajiwa kunufaika na mradi wa ugawaji wa miche hiyo na mikoa itakayonufaika ni Mbeya, Ruvuma na Songwe ambayo ni wazalishaji kahawa katika ukanda huo.

Mratibu wa Mradi wa kuendeleza zao la Kahawa (CODE-P) kutoka katika Shirika la Agroforestry, Gelvas Chiza, aliyasema hayo juzi wilayani Rungwe wakati wa ziara ya maofisa mbalimbali kutoka katika wizara za kisekta ambao walikuwa wanatembelea miradi.

Miradi waliyotembelea ni inayotekelezwa kupitia Programu ya Uboreshaji wa Mnyororo wa Thamani wa Kahawa, Chai na Mazao ya Bustani (AGRI-CONNECT) ambayo inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU).

Chiza alisema mradi huo pia unalenga kuimarisha lishe katika kaya ili kuhakikisha watoto wanakuwa na akili na uwezo mzuri wa kufanya kazi wakiwa wakubwa.

Alisema katika kutekeleza mradi huo wanashirikiana na vyama mbalimbali vya ushirika na mradi huo mpaka sasa umetekelezwa kwa muda wa miaka miwili tangu walipoanza.

Alisema mpaka kufikia Mei, mwaka huu, walikuwa wameshazalisha miche zaidi ya milioni 3.8 na wanaendelea kuisambaza na kuipanda kwa wakulima ili kuhakikisha lengo linatimia.

"Tunafanya kazi ya kuzalisha hii miche kwa kushirikiana na AMCOS mbalimbali, lengo letu ni kufanya kazi na AMCOS 50, lakini lengo letu ni kufikisha 60 na miche ambayo tunazalisha ni aina ya Compact ambayo ni bora," alisema Chiza.

Alisema miche hiyo imefanyiwa utafiti na kubainika kuwa na ubora kwa sababu inaanza kuzaa baada ya miaka miwili hali ambayo inasaidia wakulima hasa vijana kuanza kushawishika kuingia kwenye sekta hiyo ya kilimo.

Alisema miche hiyo inayozalishwa imefanyiwa utafiti na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (TACRI) na kuzalishwa kupitia AMCOS ambazo zinapatiwa elimu na vifaa vya kuzalishia miche hiyo.

Baadhi ya wakulima wanaonufaika na mradi huo walisema kwa sasa zao hilo limeanza kuwanufaisha kwa kupata mavuno na wamesaidiwa vitu mbalimbali vya kuzalishia na kulikausha.

Mwenyekiti wa Mpumisa AMCOS, Rashid Mwakyosa, alisema mbali na kusaidiwa miche, lakini wamesaidiwa kuboresha miundombinu ya kusafishia na kukaushia kahawa kwenye eneo lao.

Alisema kwa sasa ubora wa kahawa wanayozalisha umeanza kuongezeka na wana uhakika hata soko la zao hilo litakuwa bora ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Alisema wamejengewa miundombinu ya maji kwa ajili ya kusafishia kahawa, kuboreshewa mashine za kukoboa kahawa hiyo pamoja na maeneo ya kuchambulia ili kuiweka katika madaraja mbalimbali.

"Tunawashukuru hawa wenzetu wa mashirika ambao wametusaidia kwenye zao hili, vijana wetu wameanza kuingia kwenye kahawa wameanza kuachana na kazi za bodaboda ambazo zimekuwa zikiwafanya wanakuwa wazembe," alisema Mwakyosa.

Alisema wanashirikiana na mashirika mbalimbali likiwamo Shirika la Café Afrika ambalo limewasaidia nyavu za kuanikia kahawa pamoja na maturubai.

Mwakilishi wa Wizara ya Kilimo, Daines Mtei, alipongeza mashirika mbalimbali yanayotekeleza miradi ya AGRI-CONNECT kwa utekelezaji mzuri wa miradi na miradi mingi iko vizuri.

Aliwataka waendelee kusimamia vizuri miradi hiyo ili kuhakikisha wafadhili wanaridhika na kuendelea kufadhili miradi hiyo.



Wakulima wa kahawa wa Chama cha Wakulima cha Mpumisa AMCOS wilayani Rungwe mkoani Mbeya, wakianika kahawa kwenye vichanja vya kisasa ambavyo wamesaidiwa na mradi wa kuendeleza zao hilo (CODE-P), ambao ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya uboreshaji wa kahawa, chai na mazao ya bustani (AGRI-CONNECT). **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mbunge kutumia michezo kuhamasisha sensa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, amewataka wananchi wa jimbo hilo kushiriki kwenye Sensa ya Watu na Makazi ili kuisaidia serikali kupata idadi halisi ya wananchi wake.

Njeza aliyasema hayo juzi katika Kata ya Inyala wakati wa mkutano wa hadhara wa kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye shughuli za maendeleo.

Alisema ili kuhamasisha zaidi wananchi kushiriki, atatumia mbinu nyingine ikiwamo michezo ili kuhakikisha makundi yote ya wananchi yanashiriki.

Alisema sensa itasaidia serikali kutekeleza miradi ambayo inatosheleza mahitaji ya wananchi wake katika maeneo husika na endapo baadhi ya watumiaji wa huduma hizo hawatahesabika, kuna hatari huduma hizo zikawa bado hazitoshelezi.

Njeza alisema siku ya sensa wakati maofisa wakipita kwenye kaya watatakiwa kuwakuta watu sahihi wenye uwezo wa kutoa taarifa ambazo zitakuwa sahihi kuhusu familia husika ili kusiwe na upotoshaji wa taarifa.

"Serikali inapotuletea maji ni lazima ijuwe inatuletea maji kiasi gani kulingana na idadi yetu, tunapotaka shule ni lazima serikali ijue idadi ya watoto wetu, kwa hiyo ndugu zangu nawaomba sana mjitokeze siku hiyo na mhesabiwe," alisema Njeza.

Alisema atatembelea kata zote za halmashauri hiyo kuhamasisha sensa hiyo na ataanzisha ligi ambazo zitafanyika katika maeneo yote ya jimbo lake.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alimpongeza Njeza kwa kuhamasisha zoezi hilo huku akiwataka viongozi wengine wakiwamo madiwani kushiriki kuwahamasisha wananchi kwenye maeneo yao.

Alisema sensa ni muhimu kwa taifa na kwamba serikali imewekeza rasilimali nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi hilo na kusisitiza kuwa kila Mtanzania anatakiwa kuhesabiwa.

# Walalamikia viongozi ushirika tuhuma ufisadi ujenzi wa vyoo

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANACHAMA wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Mpunga Kata ya Madibila Wilaya ya Mbarali mkoani hapo, wamewalalamikia viongozi wa chama hicho wakidai kuwa wamefanya ufisadi kwenye ujenzi wa vyoo na ununuzi wa mtambo.

Wakizungumza kwenye mkutano mkuu wa kupitisha bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, walisema Bodi ya Chama hicho imeshindwa kusimamia mapato na matumizi ya chama, huku miradi ikijengwa chini ya kiwango na kuwataka viongozi hao kuwajibika.

Kabla ya kuanza mkutano huo, wajumbe walitaka kujadili suala la ubadhirifu wa fedha katika ujenzi wa vyoo ili kujiridhisha kabla ya kupitisha bajeti hali ambayo ilizua mvutano baina ya wanachama na viongozi.

Mmoja wa wanachama hao, Silvanus Ninde, aliomba ukaguzi na kubaini kuwa kuna ubadhirifu katika miradi ya ujenzi wa choo kwenye mashamba pamoja na ununuzi mtambo (greda).

"Pesa nyingi tumekatwa kwa ajili ya ujenzi wa vyoo pamoja na kuboresha miundombinu kwenye shamba letu, lakini mkaguzi alishabaini kuwa vyoo vimejengwa chini ya kiwango sasa nashanga leo mnataka tupitishe bajeti wakati bado kuna ubadhirifu," alihoji Ninde.

Naye Erick Ngeliama, alisema kwa muda mrefu viongozi wameshindwa kusimamia ushirika huo kwa maelezo kuwa kuna ubadhirifu mkubwa umefanywa katika mradi wa ununuzi wa mtambo wa kuchimbia mifereji ya maji.

Diwani wa Kata ya Madibila, Juma Msimwaya ambaye ni mjumbe katika kikao hicho, aliwataka wajumbe kuheshimiana kutokana na kutumia lugha kali dhidi ya wajumbe wa bodi huku akiwataka kuwa na ushahidi wa tuhuma wanazozitoa kwa wajumbe wa bodi.

"Hao viongozi mnaowatuhumu wanashirikiana na wajumbe na viongozi muwe mnatoa na uthibitisho hatuwezi kuendekeza matusi sababu tumeumbwa kusema," alisema Juma.

Hata hivyo, baada ya mvutano wa muda mrefu hatimaye mkutano huo ulikubaliana kuendelea kupitisha bajeti huku hoja ya ubadhirifu wa fedha ikiwekwa kiporo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Muda wa MAMCOS hiyo, Apron Kinyangasi, aliwataka wanachama wa chama hicho kuwa wavumilivu wakati jambo hilo likishughulikiwa.

Alisema wakati wa mkutano mkuu wa dharura utakaoitishwa hivi karibuni watasomewa taarifa ya gharama za ujenzi wa vyoo na ununuzi wa mtambo ili kuondoa sintofahamu iliyotokea.





# Wenye siasa za chuki, utengano watakiwa kupuuzwa

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wametakiwa kupuuza siasa za chuki na utengano na kwamba waendelee kushikamana kwa kudumisha amani na utulivu ulioko nchini.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar Dk. Abdulla Juma Mabodi, katika ziara yake ya kuimarisha uhai wa chama hicho Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema kuna baadhi ya wanasiasa wa vyama vya upinzani wakitoa kauli zisizofaa kwa kubeza hatua za maendeleo zilizofikiwa nchini, vitendo vinavyotakiwa kukemewa kabla havijahatarisha amani ya nchi.

Dk. Mabodi alisema CCM imekubali maridhiano ya kisiasa kwa nia ya kudumisha amani, mshikamano na umoja kwa wananchi wote ili serikali itoe huduma bora kwa wananchi bila kujali tofauti zao za kisiasa.

Alisema chama hicho kitaendelea kuheshimu maridhiano hayo ya kisiasa ambayo yapo kikatiba huku kikiwahimiza wananchi kuishi kwa upendo na amani kwa maslahi ya ustawi wa maendeleo endelevu.

"Kuna baadhi ya wanasiasa bado hawataki kubadilika wameshikilia historia ya siasa chafu zilizopitwa na wakati, sisi tunaendelea kuwashauri wananchi wawapuuze na kulinda amani iliyoko nchini.

Alisema hivi karibuni walisikika baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wakibeza miundombinu ya ujenzi wa miradi mbalimbali ikiwamo masoko ya kisasa na majengo ya umma.

Naibu Katibu Mkuu huyo, alisema amani ya Zanzibar imejengwa kwa gharama kubwa na CCM haiwezi kufumbia macho vitendo vya kurejesha nchi katika machafuko.

Alisema kuwa chama kimejipanga kushinda kwa zaidi ya asilimia 80 katika uchaguzi mkuu ujao kutokana na utekelezaji mzuri wa ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025.

Aliwasihi wana-CCM kutumia vizuri fursa ya uchaguzi unaoendelea hivi sasa ndani ya chama, kwa kuwachagua viongozi bora na wenye maono, uwezo na uadilifu wa kulinda maslahi yake.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mberwa Hamad Mberwa, alisema wana-CCM katika mkoa huo wanaunga mkono hatua za kimaendeleo zilizofikiwa na serikali zote mbili chini ya uongozi wa Rais Samia na Rais Dk. Mwinyi.

Alisema Mkoa wa Kaskazini Pemba ni miongoni mwa maeneo yanayoneemeka kwa utekelezwaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za kilimo, miundombinu ya barabara, utalii, uvuvi, afya na elimu.

# ADA-Tadea yawataka wafuasi wake kushiriki katika sensa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha ADA-Tadea, Juma Ali Khatib, amewataka wafuasi wa chama hicho na wananchi wote kujitokeza katika sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu, bila ya kujali itikadi zao za kisiasa kwa sababu ni muhimu kwa maendeleo.

Aliyasema hayo jana wakati akitoa elimu ya ushiriki wa sensa kwa wanachama wa chama hicho huko katika ofisi zake Kwamchina, mjini hapo.

Aliwataka wananchi kubaki katika nyumba zao siku hiyo wakati makarani wa sensa wakipita katika kaya zote na kutoa taarifa zote zinazohitajika.

"Nawaomba wanachama na wafuasi wa Chama cha ADA-Tadea kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kuhesabiwa hatua ambayo itaiwezesha serikali kupata taarifa zote muhimu zinazohitajika kwa ajili ya mipango ya maendeleo," alisema.

Alisema wanachama wa chama chake wapo tayari kuhesabiwa kwa sababu wanafahamu malengo ya sensa ya watu na makazi ambayo huiwezesha serikali kujua idadi kamili ya watu wake na kuwa tayari kuwafikishia huduma muhimu za maendeleo.

Aidha, alisema sensa ndiyo utaratibu pekee unaotumiwa na nchi zote duniani kufikisha huduma za maendeleo kwa wananchi wake kwa kuwatambua.

Halima Abdalla, Kaimu Naibu Katibu Mkuu Mwenezi wa chama hicho, aliwataka wanawake kutumia fursa ya kushiriki katika sensa ambayo itaiwezesha serikali kujua idadi kamili ya wanawake pamoja na mahitaji yao.

Alisema, hivi sasa serikali ipo katika mikakati ya kuwawezesha na kuwafikia wajasiriamali wote wanawake na njia pekee ya kufanikisha kazi hiyo ni kujulikana idadi yao ili mipango ya fedha iweze kuwafikia.

"Nawaomba wanawake wote wa Chama cha ADA-Tadea na wengine kwa ujumla kujitokeza kwa wingi kushiriki katika zoezi la sensa ya watu na makazi ambalo ni muhimu litakalowezesha taifa kujua idadi kamili ya watu wake kwa mipango ya maendeleo," alisema.

Kwa upande wake, Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi, Balozi Mohamed Hamza, aliwapongeza viongozi wa vyama vya siasa kwa utayari wao wa kushiriki zoezi hilo na ndiyo maana serikali imewashirikisha kikamilifu katika maandalizi yake.

Alisema, vyama vya siasa ndiyo vyenye wafuasi ikiwamo wanachama na ushirikishwaji wao ni muhimu kufanikisha sensa.



Mwenyekiti wa Chama cha ADA-TADEA, Juma Ali Khatib, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu ushiriki wa sensa ofisini kwake Mtaa wa Kwamchina Mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaanzisha kampuni kusimamia kilimo cha mwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuleta mageuzi makubwa ya kilimo cha mwani, Serikali ya Zanzibar imeanzisha kampuni ya mwani ambayo itasimamia maendeleo ya kilimo hicho.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Suleiman Makame Masoud, wakati alipozungumza na wadau wa kilimo hicho katika kongamano la kuelekea Siku ya Maadhimisho ya Kilimo cha Mwani huko Maruhubi mjini Unguja.

Alisema, lengo ya kuanzishwa kwa kampuni hiyo ni kutafuta masoko mapya ya kilimo hicho kwa ajili ya kuongeza kipato kwa wakulima pamoja na kufanya kazi za utafiti ili kukiendeleza kibiashara.

Alisema kwa muda mrefu kilimo cha mwani kimekuwa kikishughulikiwa na wafanyabiashara binafsi na kuibua malalamiko makubwa kwa wakulima wenyewe ikiwamo kuyumba kwa bei kutoka kwa wakulima na kuwakatisha tamaa.

"Hizo ndizo sababu kubwa zilizopelekea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Mwinyi kuunda kampuni itakayosimamia maendeleo ya kilimo cha mwani visiwani humu," alisema.

Alizitaja sababu zingine za kuundwa kwa kampuni hiyo ni kufanya kazi za usarifu na kuongeza thamani ya zao hilo kwa ajili ya kuwapo kwa matumizi mengine ya ziada.

"Changamoto kubwa zinazokikabili kilimo cha mwani kwa sasa ni kuibuka kwa maradhi mbalimbali ambayo yamekuwa yakisababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi na kilimo hicho kuyumba uzalishaji wake na kuwakatisha tamaa wakulima wake," alisema.

Waziri wa Maendeleo ya Biashara na Viwanda, Omar Said Shaaban, alisema serikali ipo katika hatua za mwisho wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya zao hilo ambacho kinatarajiwa kujengwa Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 2.6 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hicho ambacho matarajio makubwa ni kuongeza thamani ya bei ya mwani na kuleta tija kwa wakulima.

"Maandalizi ya ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya zao la mwani kipo katika hatua za mwisho...kiwanda kitajengwa Chamanangwe, Mkoa wa Kusini Pemba katika maeneo yaliyotengwa ya viwanda," alisema.

Baadhi ya washiriki wa kongamano hilo waliitaka kampuni hiyo inayomilikiwa na serikali kuja na mikakati mipya ya kuimarisha zao hilo pamoja na kutafuta masoko yenye tija.

Suleiman Batashi anayemiliki kampuni ya Sea Weed, alisema uzalishaji wa zao la mwani umeshuka kwa sababu wakulima wengi wamepoteza ari kutokana na kilimo hicho kukabiliwa na kero mbalimbali zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Ujio wa kampuni ya mwani matarajio yetu utakuja na jawabu sahihi la kuongeza bei ya zao hilo katika soko la dunia na kuingiza kipato kikubwa kwa wakulima wetu," alisema.

Mkulima wa mwani kutoka Kijiji cha Paje, Mkasi Vuai, aliitaka kampuni hiyo kuja na mikakati madhubuti itakayoamsha ari ya wakulima kuzalisha zao hilo kwa wingi wenye thamani katika soko la dunia. "Wakulima wengi tumekata tamaa kulima mwani kutokana na bei ndogo ya kilo moja Sh. 500 ambayo imepitwa na wakati kutokana na ugumu wa kilimo hicho," alisema.

Zanzibar inashika nafasi ya nne ya uzalishaji wa mwani duniani kwa kufikisha tani 11,000 na kushuka uzalishaji wake duniani, nchi za Indonesia, Philippine pamoja na Malaysia zinaongoza kwa uzalishaji wake katika soko la dunia.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SEIF SELEMAN RASHID** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN PATROL** yenye usajili namba **T477 BFH,** CHASSIS NAMBA: **JNITCSY61Z0557816** na ENGINE NAMBA: **TD42183439.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **KW/RB/3746/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BEATHER SENGEREMA KISHUSHU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAUM** yenye namba za usajili **T919 DFM** chasis namba **NCZ200028656,** engine namba **INZA945436,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/317386/2022**

## TANGAZO KUPOTELEWA KWA PASIPORT YA KUSAFIRIA



**GULAM OMARY RENDI'S** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA PASSPORT YAKE YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA TAE392303 ,ILIYOTOLEWA NA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI-UHAMIAJI MWAKA 2021, KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA GULAM OMARY RENDI'S KWA SIMU NAMBA 07183 77898

RB NAMBA/ **DSM/PHQ/RB/281794/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......17/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: YANANDE SWAI MATIKILA WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA CLAUD MARISANI MATIKILA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 13 Mwezi 09 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 11 mwezi 08 mwaka 2022**

HAKIMU

**HAKIMU MFAWIDHI**

**Magistrates Court( Approved Forms For the Primary Court)**
**GN. NO 943(Contd.)**
**FOMU MIRATH -2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**
**Usimamizi wa mirathi Na 151 /2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU GLORY IDD URASSA WA SOWETO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUWA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ADAM IDD URASSA**

**TANGAZO**
***(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hovyo mnamo tarehe 26 Mwezi 08 Mwaka 2022 Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo,

Zingatia :

Endapo kuna mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na wawea kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia

**Imetolewa leo tarehe 11 Mwezi 08 Mwaka 2022**

HAKIMU

MTENDAJI KATA YA SOWETO MANISPAA YA MOSHI Tarehe...11/8/2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......45/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: DAVID KAYANDA PEPA WA MTAWALA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA MAGRETH DAVID PEPA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 25 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 10 mwezi 08 mwaka 2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA SONGEA**
**RUFAA ARDHI NA 2.YA MWAKA 2022**
**RASHID SHAIBU MUSSA...MWOMBA RUFAA**
**DHDI YA**
**REHEMA FIDDU SHAIBU**
**NA WENZAKE WATANO.............WAJIBU RUFAA.**
**WITO WA KUITWA SHAURINI**

**KWA.**
**1.RAJABU SWAI**
**2.AJIBU HEMEDI**
**3.BONIFACE JOEL**
**4.SADIQ SELEMANI**

**POPOTE ULIPO**

Hii ni kukutaarifu kwamba shauri la rufaa tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa tarehe 18 mwezi agosti mwaka 2022 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mhe.jaji U.E.Madeha wa mahakama kuu kanda ya songea.kwahiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria .endapo hutahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi shauri hilo la rufaa litasikilizwa bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 25 mwezi julai mwaka 2022.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**SONGEA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA BUKOBA**
**MAOMBI NA 12/2022**
**YANAYOTOKANA NA KESI YA KUHUJUMU UCHUMI Na 14/2021 Ya Resident magistrate Court Bukoba)**
**DIRECTOR OF PUBLIC ROSECUTION ....................MUOMBAJI**
**DHIDI**
**YASIR AZMI**
**RESPICIUS ABEL RUCHANGULA } WAJIBU MAOMBI**
**AFIDHU ABDUL KALUGIRA }**

**WITO/KUITWA SHAURINI.**

**Kwa' YASIR AZMI**
**Popote ulipo**

Hii nikukutaarifu kwamba shauri la Mambi ya rufaa tajwa juu imepangwa
Kusikilizwa tarehe **18 mwezi Agosti mwaka 2022 saa 3.00** asubuhi, mbele ya
**MH.Jaji KILEKAMAJENGA** wa Mahakama Kuu, Kanda ya Bukoba.
Kwa hiyo, unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako Anayeruhusiwa kisheria. Endapo hutohudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi Wako shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo .
Imetolewa kwa mkoni wangu na chapa ya mahakama leo hii **tarehe 9 mwezi Agosti mwaka 2022.**

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**BUKOBA.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EVA YISAMBI MWAMAHONJE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1420/0043 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KAYUKI SECONDARI SCHOOL mwaka 2019** .kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DOD/DOD/RB/256659/2022**

**Magistrates Court( Approved Forms For the Primary Court)**
**GN. NO 943(Contd.)**
**FOMU MIRATH -2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**
**Usimamizi wa mirathi Na 150 /2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU IDD IZACK URASSA WA SOWETO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUWA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ADAM IDD URASSA**

**TANGAZO**
***(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hovyo mnamo tarehe 22 Mwezi 08 Mwaka 2022 Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo,

**Zingatia :**

Endapo kuna mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na wawea kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia


**Imetolewa leo tarehe 12 Mwezi 08 Mwaka 2022**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO MOSHI - MJINI

MTENDAJI KATA YA SOWETO MANISPAA YA MOSHI

## KUPOTEA KWA CHETI



**ATHUMANI RAJABU MKOMBOLA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P1619/0035** kilichotolewa na VICTORY SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHA/RB/ 307234/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RONALD NAFUTAL MUNUO** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T247 CUT** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI CHA KARIBU

TAARIFA:- **ARU/ARU/RB/322529/202**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENJAMIN JOHN RAY** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI **(NISSAN-XTRAIL)** yenye namba za usajili **T 896 DQJ** Chasis Namba: **NT31014356** Engine Namba: **MR0506383A**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/316880/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THOBIAS GWESO WAMBURA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Toyota yenye namba za usajili **T648BJG,** Chasis namba **Gx1106013916** na Engine namba **1G6841614**

Kwa yeyote atakayeiona au kuiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Taarifa ya polisi: **MAN/HAN/RB/274155/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na.50/2022**
**Jina la mdai DINAH ABDALLAH NJOVU**
**Jina la mdaiwa DOTTO HAMISI SHOMARI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa DOTTO HAMISI SHOMARI**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**

**MADAI YA TALAKA NA MATUNZO YA WATOTO**
Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii Tarehe 23/08/2022 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikidhibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
**Hati hii yatolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15/08/2022.**

HAKIMU

PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

# OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HABARI KIMATAIFA

## China yakasirishwa wabunge Marekani kuizuru Taiwan

**BEIJING,** CHINA

UJUMBE wa wabunge watano wa Marekani umekutana na Rais wa Taiwan, Tsai Ing-Wen mjini Taipei na kuibua hasira kwa China.

Ziara ya wabunge hao imefanyika wiki mbili tu baada ya ziara ya Spika wa Bunge la Marekani Nancy Pelosi.

Wizara ya ulinzi ya China ilisema ziara hiyo inafichua sura ya Marekani kama mzua vurugu na mhujumu wa amani katika rasi ya Taiwan.

China imetangaza kuwa itaanzisha tena luteka za kijeshi kuanzia jana kufuatia ziara ya wabunge hao wa Marekani. Nchi hiyo inakichukulia kisiwa hicho kama himaya yake na imeapa siku moja kukitwaa, lakini Taiwan inajitambua kama taifa huru na la kidemokrasia.

**DW**

## Watu 41 wafariki kwa moto Misri

**CAIRO,** MISRI

WATU 41 wakiwamo watoto 15 wamekufa katika mkasa wa moto uliozuka ndani ya kanisa moja la wakristo wa madhehebu ya Coptic wakati wa ibada jana. Watu wengine 16 walijeruhiwa wakiwamo polisi wanne waliohusika katika juhudi za uokoaji.

Mamia ya watu walijitokeza kutoa heshima za mwisho wakati wa ibada ya mazishi iliyofanyika kwenye makanisa mawili mjini Cairo.

Mkasa huo wa moto, ambao mamlaka zilisema ulitokana na hitilafu ya umeme, ulitokea kwenye kanisa la Abu Sifin lililoko katika wilaya yenye idadi kubwa ya watu wa Imbaba nje kidogo ya mji wa Cairo.

Wakristo wa Misri wanachangia asilimia 10 ya watu milioni 103 wa taifa hilo na wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu kubaguliwa na Waislamu walio wengi.

Tukio hilo la jana limekuwa moja ya majanga mabaya zaidi ya moto katika miaka ya hivi karibuni nchini Misri.

**DW**

## Usalama ulivyoimarishwa Kenya wakati matokeo yakitangazwa

**NAIROBI,** KENYA

USALAMA uliimarishwa nchini Kenya ukiwamo ndani na nje ya ukumbi wa Bomas unaotumiwa kama kituo cha kitaifa cha kujumlisha kura za urais kabla ya kutangazwa kwa matokeo ya urais.

Kuanzia majira ya asubuhi ya jana maofisa zaidi wa polisi waliingizwa katika ukumbi huo ili kuimarisha usalama wakati Tume ya Uchaguzi na Mipaka IEBC ikijiandaa kumtangaza mshindi wa uchaguzi wa urais ambaye William Ruto akishinda kinyang'anyiro hicho cha kiti cha urais.

Wakati huo huo, meza zote za uhakiki wa matokeo ya kura zikibaki tupu, huku eneo la wanadiplomasia lilikaliwa na watu wengine kinyume na siku za nyuma.

Tangu watu wapige kura Jumanne iliyopita na kuwachagua viongozi wao matokeo ya nafasi nyingine tano zimeshatolewa, huku nafasi ya rais ikiwa ishapata mrithi wake.

Hata hivyo hamu ya wengi ilikuwa ikielekezwa katika ukumbi wa Bomas ambako kura za urais zilikuwa zikijumlishwa na matokeo kutangazwa rasmi.

Kwa kawaida jana huwa siku ya shughuli nyingi katika maisha ya kila siku ya raia, wengi waliacha kwenda kazini na kubaki nyumbani na baadhi ya wafanyabiashara walifunga maduka yao.

Kila mwananchi wa Kenya ni kana kwamba ametekwa nyara na matokeo ya uchaguzi wa urais.

Wengi walitaka mshindi atangazwe ili waendelee na shughuli zao. Katika mji wa Eldoret, eneo la Rift Valley linalochukuliwa kama ngome ya Naibu wa William Ruto, mvua ilinyesha usiku kucha na wenyeji hawana kasi ya kuamka.

'Mwendo ni wa pole pole hapa, kwa kawaida watu hudamka alfajiri na mapema kuendelea na shughuli za kawaida lakini leo hali ni tofauti," alisema mwandishi wa BBC Robert Kiptoo.



Anaongeza kuwa juzi Jumapili kulikuwa na shughuli mjini lakini huenda pia zilinoga kwa sababu ilikuwa ni mwisho wa wiki. Katika mji wa Kisumu, magharibi mwa Kenya ambako ni ngome ya aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga, wenyeji walikuwa na hamu kubwa ya kutaka matokeo kutangazwa.

Baada ya watu kupiga kura wenyeji walikuwa wakikusanyika katika vikundi kujadili na kusikiliza kupitia redio kuhusu kinachoendelea.

**BBC**


EAGLE RECOVERIES LIMITED

**NOTISI/MNADA**

KWA NIABA YA **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED WA S. L. P. 110183, DAR ES SALAAM.** TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI KWA WADAIWA WALIO TAJWA HAPA CHINI WALIPE MADENI YAO WANAYODAIWA KWA MUDA MREFU, ENDAPO WATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA. DHAMANA ZAO ZITAUZWA KWA RATIBA IFUATAYO.

| NA. | JINA LA MDAIWA | MALI INAYOUZWA | MAHALI ILIPO MALI INAYOUZWA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | CHALICHA ELECTRONICS & SOLAR SUPPLIES COMPANY LIMITED/MWIKWABE CHALICHA MATIKU | NYUMBA YENYE HATI NA.28402, KIWANJA NA.770, KITALU NA." BIX" YENYE SQM 450 | ENEO LA MKUYUNI, WILAYA YA NYAMAGANA, MWANZA | IJUMAA 02/09/2022 |
| 02 | CHALICHA ELECTRONICS & SOLAR SUPPLIES COMPANY LIMITED/MWIKWABE CHALICHA MATIKU | NYUMBA YENYE HATI NA.51833, KIWANJA NA.771, KITALU NA." BIX" YENYE SQM 450 | ENEO LA MKUYUNI, WILAYA YA NYAMAGANA, MWANZA | IJUMAA 02/09/2022 |
| 03 | ALEX DUKE | NYUMBA YENYE HATI NA.65633, KIWANJA NA.1009, KITALU NA." E" YENYE SQM 534 | ENEO LA BUHONGWA, WILAYA YA NYAMAGANA, MWANZA | JUMAMOSI 03/09/2022 |

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mnada utafanyika sehemu ilipo dhamana
3. Mnunuzi atakayefika bei ya juu atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya mnada
4. Endapo mteja atashindwa kumaliza 75% ndani ya siku 14 kiasi kilichotolewa awali 25% hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
5. Baada ya kukamilisha malipo yote ni jukumu la mnunuzi kumuhamisha mkazi/wakazi waliopo ndani ya dhamana husika.
6. Gharama za kubadilisha hati miliki (Transfer of ownership) pamoja na gharama nyingine ni juu ya mnunuzi.Wote mnakaribishwa

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**EAGLE RECOVERIES LIMITED,**
**S.L.P 34462,**
**DAR ES SALAAM,**
**SIMU NA.0758 784 432/ 0757 186 767 /0743 448 888**
**EMAIL: eaglerecoveries2017@gmail.com**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**EQUITY BANK(TANZANIA)LIMITED,**
**S.L.P 110183,**
**GOLDEN JUBILEE TOWER, DAR ES SALAAM.**
**SIMU NA. +255 768 985 500**
**EMAIL: info@equitybank.co.tz**
**WEB: www.equitybank.co.tz**

116994602


## Putin aapa kuimarisha uhusiano Korea Kaskazini

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amesema ameapa kuimarisha uhusiano wake na Korea Kaskazini.

Katika barua iliyotumwa kwa kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong un katika maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa Pyongyang, Putin alisema hatua hiyo itakuwa kwa maslahi ya nchi zote mbili.

Kwa upande wake, Kim alisema urafiki kati ya mataifa yote mawili ulianza katika Vita vya Pili vya Dunia na ushindi dhidi ya Japan.

Aliongeza kuwa uhusiano wao wa kirafiki utaimarika zaidi.

Kulingana na ripoti ya chombo cha habari cha serikali ya Korea Kaskazini KCNA, Putin alisema uhusiano huo ulioimarishwa utaendana na maslahi ya nchi hizo mbili.

Katika barua yake, Kim alisema urafiki wa Russia na Korea Kaskazini ulioanzishwa katika vita dhidi ya Japan umeimarishwa na kuendelezwa karne baada ya karne.

Iliongeza ushirikiano wa kimkakati na wa kimbinu, uungaji mkono na mshikamano kati ya nchi hizo mbili umewekwa kwenye hatua mpya ya juu, katika mstari wa pamoja kwa ajili ya kukatisha tamaa tishio la kijeshi la vikosi vya uhasama na uchochezi.

Korea Kaskazini haikutambua majeshi hayo kwa majina, lakini neno hilo limetumiwa mara kwa mara na nchi hiyo kuilenga Marekani na washirika wake.

Umoja wa Kisovyeti ulikuwa mshirika mkuu wa Korea Kaskazini, ukitoa ushirikiano wa kiuchumi, mabadilishano ya kitamaduni na misaada.

**BBC**




EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA UTOAJI WA WAANGALIZI WA MAMALIA NA UFUATILIAJI WA SAUTI WA BAHARINI**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0001-00**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, ununuzi na Ujenzi wa Gati na Vifaa vya Kupakia katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu yenye uzoefu kueleza nia yao kwa:

**Waangalizi wa mamalia na ufuatiliaji mwangwi na Sauti wa baharini (Passive Acoustic Monitoring-PAM).**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufuo wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni, eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**
BESIX Ballast Nedam Limited itatekeleza kwa muda wote wa mradi (Januari 2023 hadi Juni 2024) itifaki ya kupunguza athari kwa mamalia wa baharini na kelele zitokanazo na kazi ya usimikaji wa nguzo za Gati. Itifaki hii ni pamoja na:
- Utekelezaji wa uchunguzi wa mamalia wa baharini (Marine Mammal Observation - MMO) kabla na wakati wa operesheni ya kusimika nguzo
- Utekelezaji wa ufuatiliaji wa Sauti (Passive Acoustic Monitoring-PAM), Ugunduzi wa mamalia wa baharini karibu eneo la kazi.

**Ili kusaidia utekelezaji wa vipengele hivi viwili, BESIX Ballast Nedam Limited inatafuta:**
- Vifaa vya ufuatiliaji wa sauti (PAM equipment)
- Waangalizi wa mamalia wa baharini wenye uzoefu na waendeshaji wa ufuatiliaji wa sauti baharini na/au
- Huduma za mafunzo ya ufuatiliaji mamalia wa baharini na uwezekano wa kufanya mafunzo kwenye kwenye eneo la mradi

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

**Kwa vifaa vya ufuatiliaji wa sauti (PAM equipment)**
- Mbinu ya kupeleka vifaa
- Sifa za kitaalamu
- Usaidizi wa kiufundi wakati wa ufungaji vifaa na wakati wa operesheni

**Kwa waangalizi wa mamalia wa baharini na waendeshaji wa vifaa vya Sauti**
- CV,
- Uzoefu katika miradi kama hiyo
- Cheti cha mafunzo (ikiwezekana JNCC au kinachofanana)

**Kwa huduma za mafunzo ya MMO na PAM**
- CV na sifa za wakufunzi
- Mpango wa mafunzo
- Kutambuliwa na mashirika ya kimataifa (JNCC au kinachowiana)
- Uwezekano wa kutoa mafunzo na kufundisha waendeshaji wadogo wa MMO / PAM kwenye eneo la kazi wakati wa ujenzi

**Pia BBN itazingatia:**
- Kanuni za petroli na matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unashauriwa.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa procurement@bbnjv.com. **(Ukubwa wa Barua Pepe: MB 20 & Viambatanishi vyote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **tarehe 30 Agosti 2022 , Saa 6 mchana kwa saa za Tanzania.**

Makampuni yanayokidhi vigezo yatatathminiwa na ikiwa yatachaguliwa, yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka** : Kampuni zilizokidhi matakwa ya mchakato wa awali wa mchujo pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni zao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

216993401

# IYANII, COSTA TITCH 'WADATISHA' USIKU WA NMB FULL MOON PARTY

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WASANII wa muziki, Ian Oure Okwemba 'Iyanii' kutoka Kenya na Costa Tsobanoglou 'Costa Titch' wa Afrika Kusini, wamekuwa kivutio kwa mashabiki waliohudhuria 'Usiku wa Full Moon Party', uliofanyika katika Fukwe za Hoteli ya Kitalii ya Kendwa Rocks, Zanzibar, ukidhaminiwa na Benki ya NMB.

Full Moon Party iliyodhaminiwa kupitia Kampeni ya NMB Fri-Yay, yenye lengo la kukuza na kuhamasisha matumizi ya kadi katika kufanya malipo yasiyohusisha pesa taslimu 'cashless' lilifanyika juzi Zanzibar, na ni onyesho la kila mwezi linaandaliwa kwa pamoja baina ya NMB na Kendwa Rocks, likichagiza matumizi ya Kadi za NMB MasterCard.

Fri-Yay, ni huduma inayotoa punguzo la asilimia 10 kwa kila muamala wa malipo utakaofanywa na mteja kwa kutumia kadi mbalimbali za NMB, katika migahawa, hoteli, 'supermarket' na vituo vya mafuta (petrol station), vikiwamo vya Puma Upanga (Viva Tower), Ocean Road na Kawe kwa Dar es Salaam.

Baada ya shoo za utangulizi kutoka kwa wasanii mbalimbali wa Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar, sambamba na burudani kali kutoka kwa Ma-DJ wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Iyanii alipanda stejini akimtangulia Rapa Msauzi Costa Titch.

Iyanii alipanda stejini majira ya saa 5:17 usiku, ambako alitumia takriban dakila 40, akipagawisha vilivyo watalii, mashabiki wa muziki na waalikwa wengine, akikonga nyoyo zao kupitia vibao vyake kadhaa vilivyojenga heshima Afrika Mashariki, vikiwamo: Furaha, Pombe, Memories, Master na kopi za wasanii wengine duniani.

Kupitia nyimbo hizo, Iyanii aliwaimbisha mashabiki waliomtii na kuimba pamoja naye na hivyo kumwongezea mzuka uliomsukuma kuvua fulana aliyovaa na kutumbuiza kifua wazi.

Iyanii alipomaliza alipanda 'Mjukuu wa Mandela' Costa Titch, ambaye alivuruga vilivyo akili za wahudhuriaji wa Full Moon Party kwenye Fukwe za Kendwa Rocks Hotel, baadhi ya nyimbo zilizovuta hisia za mashabiki ni pamoja na Big Flexa, Ma Gang, Nkalakatha, Nomakanjani, Uthini, Areyeng, Great Tik Tok, Thembi na nyinginezo.

Katikati ya dakika 35 za Costa Titch kupagawisha mashabiki, alipanda jukwaani mkali wa Bongo Fleva kutoka Lebo ya Wasafi, Mbosso Khan, ambaye alisalimia mashabiki kisha kuimba naye kwa dakika tano na kushuka jukwaani, kabla ya Msauzi huyo kuacha 'kurap' na kugeukia U-Dj, alikoporomosha vibao vikali mfululizo.

Ukiondoa Iyanii, Costa Titch na Mbosso Khan, Full Moon Party ilipambwa na burudani za wasanii na ma-Dj kutoka Zanzibar, Dar es Salaam na Arusha, wakiongozwa na DJ K Flip na DJ Mammy, ambao walisimamia mashine kuanzia saa 6:45 usiku hadi majogoo, hivyo kuwafanya mashabiki kunata kwa midundo yao hadi mapambazuko.



Msanii wa muziki, Costa Tsobanoglou 'Costa Titch' wa Afrika Kusini akisalimiana na mashabiki wakati akipiga shoo kwenye usiku wa Full Moon party uliyofanyika mwishoni mwa wiki visiwani Zanzibar. Benki ya NMB ilishiriki kama mdhamini mkuu wa sherehe hizo ambazo hufanyika kila mwisho wa mwezi. Kupitia sherehe hizo za Full Moon party, NMB inaendelea kuchagiza matumizi ya kadi kwenye manunuzi mbalimbali. **MPIGAPICHA WETU**

# Pluijm ataka pointi tatu nyumbani

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, ameweka vipaumbele vyake katika kuhakikisha wanaibuka na pointi tatu kuelekea mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu watakayocheza leo dhidi ya Tanzania Prisons katika uwanja wa nyumbani wa Liti.

Ligi Kuu Bara ilianza kutimua vumbi jana kwa michezo miwili kuchezwa ambapo Ihefu ilikuwa nyumbani Mbarali kuikaribisha Ruvu Shooting huku Namungo ikiwa mwenyeji wa Mtibwa Sugar mkoani Lindi.

Mbali na mchezo wa Singida Big Stars dhidi ya Tanzania Prisons ya Mbeya, mechi nyingine zitakazopigwa leo ni Polisi Tanzania dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha na Dodoma Jiji FC dhidi ya Mbeya City utakaopigwa Uwanja wa Liti mkoani Singida.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, alisema kuwa Plujim amewataka wachezaji wake kujitahidi kuibuka na pointi tatu katika uwanja wa nyumbani ili kujiwekea mazingira mazuri kwenye ligi.

"Kikosi chetu kipo vizuri kuelekea mchezo wetu wa kesho (leo), na hakuna majeruhi wa aina yeyote, wachezaji wote wapo fiti tayari kwa kuanza ligi.

"Kocha ameridhishwa na kikosi chake na amewataka wachezaji kuhakikisha wanafanikiwa kutwaa ponti tatu za Prisons na kila mchezo watakaocheza katika uwanja wa nyumbani ili kujiwekea mazingira mazuri katika ligi hiyo," alisema Massanza.

## Jang'ombe kusajili nyota nane wapya

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Taifa ya Jang'ombe imesema inampango wa kusajili wachezaji nane wapya ili kukipa nguvu kikosi hicho kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar 2022/23.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa timu hiyo, Haji Kiduka, alisema miongoni mwa wachezaji watakaowasajili msimu huu ni kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Alisema kwa sasa ni mapema kuweka wazi nchi ambazo wachezaji hao wanatoka na kwamba watafahamika siku ya utambulisho rasmi kabla ya kufungwa dirisha la usajili ambalo limebaki siku tano.

Alisema msimu huu wanasajili kikosi ambacho kitaleta mageuzi ya soka hasa Ligi Kuu ya visiwani hapa kwa kuwa lengo lao kubwa ni kubeba ubingwa wa ligi hiyo maarufu kama Ligi Kuu ya PBZ.

"Tumesajili wachezaji wa kufanya kazi tunayohitaji, malengo yetu ni kutwaa taji la Ligi Kuu, hivyo sisi kama 'Wakombozi Wang'ambo' lazima jambo letu liwe na litimie,"alisema.

## Yanga Princess kamili kwa msimu mpya

**Joram Gervas na Camila Bonanza**

LICHA ya kwamba tarehe rasmi ya kufunguliwa kwa pazia la Ligi Kuu ya Wanawake nchini bado haijawekwa wazi, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema wako tayari kwa msimu mpya wa ligi hiyo.

Akizunguza na waandishi wetu, Edna alisema kwa sasa kikosi chake kipo kambini kujiandaa na msimu mpya huku akibainisha kwamba imesheheni maingizo mapya ya wachezaji wenye uwezo mkubwa.

Edna alisema wameachana na wachezaji takriban 10 wa ndani na nje ya nchi kuelekea msimu mpya.

Alisema matarajio yao msimu huu ni kuwa mabingwa baada ya kuukosa kwa misimu mitatu mfululizo wakishuhudia watani wao wa jadi, Simba Queens wakitawala.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RONALDO ALIKATALIWA**
CRISTIANO Ronaldo alipewa ofa na Manchester United kwa AC Milan na Inter Milan, lakini klabu zote za Serie A zilikataa nafasi ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 37. ***(Tancredi Palmeri via Sun)***

**AUBAMEYANG KUPIGANIA NAMBA**
PIERRE-Emerick Aubameyang anataka kupigania nafasi yake katika Klabu ya Barcelona, ambayo imekataa dau la pauni milioni 12 kutoka kwa Chelsea kumnunua mshambuliaji huyo wa Gabon mwenye umri wa miaka 33. ***(Deportivo Mundo via Mirror)***

**XAVI AMTAKA MESSI**
KOCHA wa Barcelona, Xavi ameiomba Barcelona kumsajili tena mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, kutoka Paris St-Germain. ***(Sun)***

**CAICEDO AGOMBEWA**
KLABU ya Manchester United imejiunga na orodha ya Klabu za Ligi Kuu England ikiwamo Arsenal na West Ham, zinazotaka kumsajili kiungo wa kati wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 20 kutoka Brighton. ***(Mirror)***

**AOUAR AKARIBIA FOREST**
KLABU ya Nottingham Forest inakaribia kumnunua kiungo wa kati wa Lyon na Ufaransa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 24, ambaye hapo awali amekuwa akihusishwa na Arsenal. ***(Sky Sports Italy via Metro)***

**BARCA NA DAU LA AUBA**
BARCELONA wanataka ada ya pauni milioni 23 Pierre-Emerick Aubameyang, ambaye alijiunga nao Februari mwaka huu. ***(Metro via Gerard Romero)***

**SOW PIA ATAKIWA**
NOTTINGHAM Forest pia wamewasilisha dau la pauni milioni 17 kwa kiungo wa Eintracht Frankfurt na Uswizi, Djibril Sow mwenye umri wa miaka 25. ***(talkSPORT)***

**TIELEMANS NA ARSENAL**
KLABU ya Leicester City ipo tayari kuruhusu Arsenal kumsaka kiungo wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25 kuondoka bila malipo msimu ujao. ***(Times)***

**GUIRASSY AWANIWA EVERTON**
KLABU ya Everton imetoa ofa kwa mshambuliaji wa Rennes na Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 26. ***(Mail)***

**BERG ATAKIWA BLACKBURN**
KLABU ya Blackburn inaongoza harakati za kumsajili beki wa kati wa Uholanzi, Sepp van den Berg mwenye umri wa miaka 20 kwa mkopo kutoka Liverpool. ***(Sun)***

**EMERSON AULIZIWA NICE**
KLABU ya Nice imeulizia kuhusu beki wa kushoto wa Chelsea na Brazil, Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 28. ***(Fabrice Hawkins via Get French Football News)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BRUYNE ATARAJIA SILVA KUBAKI CITY

**Anapendwa sana na sisi na anajua, kwa jinsi ninavyoona, nadhani atakuwa hapa kwa hivyo...**

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Kevin De Bruyne, amesisitiza kuwa hajali nia ya Barcelona ya kumnunua Bernardo Silva, kwani anaamini hataondoka.

Kwa muda mrefu timu hiyo ya Katalunya imekuwa na nia ya kutaka kumsajili Silva na kocha Xavi amewaomba viongozi wa Camp Nou kutafuta fedha zinazohitajika ili hatimaye kumleta katika majira haya ya joto.

Silva amefanya kila awezalo kubakia katika Klabu hiyo na mashabiki wamemmwagia sifa kemkemu mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, huku wakilitaja jina lake alipotoka katika mechi ya Jumamosi wakiichapa Bournemouth mabao 4-0.

Baada ya mchezo huo, De Bruyne aliulizwa kuhusu hatima ya Silva na alisisitiza kuwa anaamini bado watakuwa pamoja mwishoni mwa mwezi huu wakati dirisha la usajili litakapofungwa.

"Nadhani anapendwa sana na sisi na anajua," alisema De Bruyne. "Kwa jinsi ninavyoona, nadhani atakuwa hapa kwa hivyo hakuna kitu ambacho nina wasiwasi nacho.

"Chochote kitakachotokea, yeye ni mzuri kwetu na ninatarajia kuwa hapa pamoja nasi mwaka huu."

Kocha wa City, Pep Guardiola ameweka wazi kuwa '100%' anataka kumbakisha Silva zaidi ya msimu huu wa majira ya joto, lakini amethibitisha hapo kwamba hatamzuia mchezaji wake yeyote ikiwa ataomba kuondoka katika klabu hiyo.

Silva mkataba wake wa sasa upo hadi mwaka 2025, kumaanisha kuwa City haitakuwa na haraka ya kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake msimu huu wa majira ya joto.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,023,

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 18 AGOSTI 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/08/22 | 19:00 | Rakow Czestochowa vs Slavia Prague | 2.73 | 3.24 | 2.53 |
| 02. 18/08/22 | 19:30 | El Gouna vs Ghazl EL Mahallah | 2.50 | 2.86 | 3.07 |
| 03. 18/08/22 | 19:30 | Al Masry Club vs Ismaily SC | 2.39 | 2.86 | 3.26 |
| 04. 18/08/22 | 20:00 | Pyunik Yerevan vs Sheriff Tiraspol | 2.83 | 3.13 | 2.52 |
| 05. 18/08/22 | 20:00 | Apollon Limassol vs Olympiakos | 3.37 | 3.22 | 2.16 |
| 06. 18/08/22 | 20:00 | CSKA Sofia vs FC Basel | 3.04 | 3.24 | 2.32 |
| 07. 18/08/22 | 20:00 | BSC Young Boys vs Anderlecht | 2.16 | 3.48 | 3.13 |
| 08. 18/08/22 | 20:00 | Maccabi Tel Aviv vs Nice | 3.02 | 3.22 | 2.33 |
| 09. 18/08/22 | 21:00 | HJK Helsinki vs Silkeborg | 2.87 | 3.22 | 2.43 |
| 10. 18/08/22 | 21:00 | SC Dnipro 1 vs AEK Larnaca | 2.63 | 3.23 | 2.63 |
| 11. 18/08/22 | 21:00 | Zrinjski Mostar vs Slovan Bratislava | 2.62 | 3.18 | 2.67 |
| 12. 18/08/22 | 21:15 | Maribor vs CFR Cluj | 3.03 | 3.13 | 2.38 |
| 13. 18/08/22 | 22:00 | Austria Vienna vs Fenerbahce | 2.78 | 3.29 | 2.46 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: DIAZ ANAWEZA KUMRITHI MANE LIVER




**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amemtaka Luis Diaz kuiga namba za ufungaji za Sadio Mane hapo kwenye Uwanja wa Anfield.

Mane aliondoka Liverpool msimu huu wa majira ya joto akiwa na rekodi ya kufunga mabao 120 katika michezo 269 na tuzo moja ya Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England, baada ya kugeuka kuwa mashine mahiri kwa miaka sita chini ya Klopp.

Diaz bado hajaweza kufikia mechi kama hizo, akiwa amefunga mabao manne katika mechi 13 za Ligi Kuu.

Alipoulizwa kama Diaz angeweza kujifunza jinsi Mane anavyofunga, Klopp alisisitiza kwamba mfumo wa soka wa Liverpool utamwezesha kufanya hivyo.

"Ni jinsi tunavyocheza," alisema Klopp.

"Ni jinsi tunavyowaleta wachezaji katika hali hii. Bila shaka ni kuhusu kama iko ndani yako au la, lakini ni jinsi tunavyocheza, jinsi tunavyoweka wachezaji, jinsi tunavyolinda wachezaji.

"Namna tunavyocheza inapaswa kuwasaidia washambuliaji, tunavyocheza tusaidie safu ya mwisho ya mabeki kwa sababu kila mmoja anahusika. Ndio maana kidogo pia viungo wa kati wanaonekana kutofunga vya kutosha, kwa sababu wanahusika katika kuweka kila kitu pamoja.

"Unaona hali ambayo Diaz alikuwa nayo nafasi kubwa na hakuwa na bahati. Yuko katika hali nzuri na hiyo ni muhimu zaidi.

"Si kwamba ninamwambia baada ya mchezo, 'Ulipaswa kufunga hapa au pale.' Vijana wanajua hilo kwa sasa. Inatokea. Ni mchakato wa kawaida.

"Mabao kumi hadi 15? Hakika huo ndio ubora wake. Tunahitaji kuona, lakini huo ndio uwezo wake. Anahitaji goli moja tu kisha tutatoka hapo."

# Ancelotti ataka zaidi kwa Tchouameni, Camavinga

**MADRID, Hispania**

AURELIEN Tchouameni na Eduardo Camavinga walishindwa kuonyesha ubora ambao wamefanya mazoezini wakati Real Madrid iliposhinda mabao 2-1 dhidi ya Almeria Jumapili, kwa mujibu wa kocha, Carlo Ancelotti.

Madrid walitoka nyuma kwa bao la mapema la Largie Ramazani kwenye Uwanja wa Power Horse katika mchezo wao wa ufunguzi wa LaLiga msimu huu, na kusawazisha kupitia Lucas Vazquez dakika ya 61.

Kisha wakaondoka na pointi zote tatu zikiwa zimesalia dakika 15 pale mchezaji wa akiba David Alaba alipofunga mkwaju wa faulo uliompita Fernando Martinez kutoka umbali wa yadi 25.

Tchouameni, alijiunga na timu hiyo akitokea Monaco kwa ada ambayo inaweza kupanda hadi euro milioni 100, na Camavinga alianza pamoja na Toni Kroos katika safu ya kati.

Nafasi yake ilichukuliwa na Luka Modric wakati wa mapumziko, wakati Tchouameni alibadilishwa na Eden Hazard.

Na baada ya mchezo huo, Ancelotti alisema: "Kwangu mimi, (Antonio) Rudiger alicheza mchezo mzuri.

"Vijana hawakucheza kama kawaida. Kwa kile wanachofanya kwenye mazoezi wanastahili kucheza. Hawajafanya chochote kibaya, lakini wanaweza kufanya vizuri zaidi.

"Nilimwondoa Camavinga kwa sababu alikuwa na kadi na ilikuwa kawaida, kwa sababu tumechanganya mchezo na makosa na ulinzi. Kuanzia hapo imetugharimu sana."

Hazard amevumilia wakati mgumu wa majeraha tangu ajiunge naye akitokea Chelsea Julai 2019, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji anatumai kuwa na jukumu muhimu msimu huu.

HABARI MICHEZO


154,178/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/08/22 | 17:00 | Crystal Palace vs Aston Villa | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 02. 20/08/22 | 17:00 | Fulham vs Brentford | 2.39 | 3.28 | 2.93 |
| 03. 20/08/22 | 17:00 | Preston vs Watford | 2.89 | 3.14 | 2.49 |
| 04. 20/08/22 | 17:00 | Birmingham vs Wigan | 2.41 | 3.18 | 2.98 |
| 05. 20/08/22 | 17:00 | Swansea vs Luton Town | 2.41 | 3.18 | 2.98 |
| 06. 20/08/22 | 17:00 | Bolton vs Sheffield Wed | 2.85 | 3.39 | 2.39 |
| 07. 20/08/22 | 17:00 | Forest Green vs Plymouth | 2.70 | 3.40 | 2.50 |
| 08. 20/08/22 | 17:00 | Burton vs Port Vale | 2.31 | 3.38 | 2.98 |
| 09. 20/08/22 | 17:00 | Doncaster vs Salford City | 2.63 | 3.28 | 2.63 |
| 10. 20/08/22 | 17:00 | Colchester vs Leyton Orient | 2.98 | 3.33 | 2.33 |
| 11. 20/08/22 | 17:00 | Crawley Town vs AFC Wimbledon | 2.43 | 3.24 | 2.89 |
| 12. 20/08/22 | 17:00 | Mansfield vs Stockport | 2.25 | 3.49 | 2.99 |
| 13. 20/08/22 | 17:00 | Dundee Utd vs St. Mirren | 2.31 | 3.09 | 3.24 |
| 14. 20/08/22 | 17:00 | Motherwell vs Livingston | 2.25 | 3.13 | 3.33 |
| 15. 20/08/22 | 17:00 | Ross County vs Kilmarnock | 2.26 | 3.14 | 3.29 |
| 16. 20/08/22 | 17:00 | St. Johnstone vs Aberdeen | 2.93 | 2.98 | 2.58 |
| 17. 20/08/22 | 17:00 | Hamilton vs Raith Rovers | 2.43 | 3.14 | 2.99 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 16 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1178 | Busan I Park vs Seoul E Land | 3.39 | 3.34 | 1.98 |
| 13:00 | 2103 | Yokohama vs Thespakusatsu | 1.66 | 3.39 | 4.92 |
| 13:00 | 2424 | Anyang vs Bucheon | 1.85 | 3.29 | 3.93 |
| 14:30 | 5852 | Shanghai SIPG vs Shenzhen | 1.58 | 3.72 | 5.09 |
| 16:00 | 3730 | Polisi Tanzania vs Young Africans | 5.68 | 3.13 | 1.65 |
| 17:00 | 1101 | Al Ahli Amman vs Kfarsoum | 1.56 | 3.78 | 5.11 |
| 18:00 | 2908 | Lokomotiv Tashkent vs Bunyodkor | 2.21 | 3.24 | 2.95 |
| 18:00 | 3363 | Jedinstvo BP vs Jezero | 2.50 | 3.04 | 2.70 |
| 18:30 | 3602 | MP Mikkeli vs FC KTP | 3.29 | 3.58 | 1.93 |
| 19:30 | 1386 | Sonderjyske vs FC Helsingor | 1.53 | 4.12 | 4.91 |
| 19:30 | 4834 | Hvidovre IF vs Fremad Amager | 1.58 | 3.78 | 4.91 |
| 19:35 | 5588 | Lekhwiya SC vs Al Rayyan SC | 1.61 | 4.24 | 4.14 |
| 20:00 | 1074 | Petrovac vs Decic Tuzi | 2.65 | 3.34 | 2.36 |
| 20:00 | 2110 | Vendsyssel FF vs Hobro | 2.07 | 3.29 | 3.19 |
| 20:00 | 2270 | Osters IF vs Orebro SK | 1.71 | 3.76 | 4.78 |
| 20:00 | 2664 | Vasteras SK vs Trelleborgs FF | 2.21 | 3.62 | 3.01 |
| 20:00 | 3389 | HB Koge vs Nykobing FC | 1.72 | 3.73 | 4.02 |
| 20:30 | 5185 | Cape Town City vs Maritzburg Utd | 1.98 | 3.01 | 4.12 |
| 21:00 | 3713 | Sutjeska vs Iskra | 1.58 | 3.83 | 4.82 |
| 21:45 | 1180 | Forest Green vs Accrington | 2.22 | 3.31 | 3.06 |
| 21:45 | 1209 | Mansfield vs AFC Wimbledon | 1.83 | 3.45 | 4.10 |
| 21:45 | 1220 | Bristol City vs Luton Town | 2.40 | 3.25 | 2.80 |
| 21:45 | 1263 | Exeter vs Wycombe | 2.50 | 3.30 | 2.65 |
| 21:45 | 1577 | Birmingham vs Watford | 3.30 | 3.30 | 2.11 |
| 21:45 | 1654 | Oxford Utd vs Lincoln | 1.81 | 3.65 | 3.95 |
| 21:45 | 1733 | Swansea vs Millwall | 2.40 | 3.14 | 2.89 |
| 21:45 | 1756 | Swindon Town vs Leyton Orient | 2.40 | 3.25 | 2.80 |
| 21:45 | 1824 | Portsmouth vs Cambridge Utd | 1.72 | 3.66 | 4.41 |
| 21:45 | 2020 | Norwich City vs Huddersfield | 1.62 | 3.60 | 5.40 |
| 21:45 | 2084 | Fleetwood Town vs Cheltenham | 2.11 | 3.40 | 3.20 |
| 21:45 | 3121 | Burnley vs Hull City | 1.56 | 3.74 | 5.78 |
| 21:45 | 3300 | Barrow vs Walsall | 2.46 | 3.04 | 2.89 |
| 21:45 | 3459 | Hartlepool vs Tranmere | 2.42 | 3.11 | 2.91 |
| 21:45 | 3794 | Grimsby vs Carlisle | 2.13 | 3.21 | 3.36 |
| 21:45 | 4260 | Crewe vs Sutton United | 2.33 | 3.26 | 2.91 |
| 21:45 | 4473 | Burton vs Ipswich | 4.30 | 3.50 | 1.78 |
| 21:45 | 4794 | Shrewsbury vs Derby | 2.99 | 3.24 | 2.29 |
| 21:45 | 4822 | Preston vs Rotherham | 1.90 | 3.30 | 4.00 |
| 21:45 | 4840 | Barnsley vs Bristol Rovers | 2.08 | 3.31 | 3.36 |
| 21:45 | 4959 | MK Dons vs Port Vale | 1.95 | 3.34 | 3.74 |
| 21:45 | 5038 | Crawley Town vs Northampton | 3.09 | 3.29 | 2.21 |
| 21:45 | 5263 | Charlton vs Plymouth | 2.23 | 3.30 | 3.05 |
| 21:45 | 5266 | Bolton vs Morecambe | 1.46 | 4.30 | 6.19 |
| 21:45 | 5820 | Newport vs Salford City | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 21:45 | 5881 | Peterborough vs Sheffield Wed | 2.60 | 3.30 | 2.55 |
| 22:00 | 1409 | QPR vs Blackpool | 2.08 | 3.36 | 3.31 |
| 22:00 | 1942 | FK Arsenal Tivat vs Mornar Bar | 2.64 | 3.13 | 2.49 |
| 22:00 | 2735 | Copenhagen vs Trabzonspor | 2.09 | 3.25 | 3.40 |
| 22:00 | 3301 | Bodo Glimt vs Dinamo Zagreb | 2.24 | 3.45 | 2.90 |
| 22:00 | 5006 | Rangers vs PSV Eindhoven | 2.50 | 3.30 | 2.65 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# NKOMA ASAKA MBINU SIMBA QUEENS KUTOBOA CECAFA

**Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema wanapaswa kujiandaa vizuri tayari kwa kukutana na timu ili kuweza kuendelea kupata matokeo kwenye michuano ya Wanawake ya kuwania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ukanda wa Afrika Mashariki, (Caf Wowen Champions League Qualifiers Cecafa Zone).

Michuano hiyo iliyoanza juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, mechi ya kwanza ilikuwa kati ya She Corporates ya Uganda ambayo iliibuka na ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Yei Joint Stars FC ya Sudan Kusini.

Katika mechi ya pili, Simba ilianza vizuri kwa kuibuka na ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Garde Republicaine FC ya Djibouti.

Wafungaji wa Simba katika mchezo huo walikuwa ni Fallone Pambani akifunga bao moja, Olaiya Barakati na Asha Djafar ambao kila mmoja alicheka na nyavu mara mbili huku Joelle Bukuru akihitimisha ushindi huo kwa kutupia la sita.

Simba Queens itashuka tena dimba kesho kucheza mechi yake ya pili kwa kuvaana na She Corporates mchezo utakaopigwa katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nkoma alisema amefurahia ushindi huo mnono, lakini wamecheza na timu dhaifu jambo ambalo atakuwa na kazi kubwa hasa watakapokutana na timu ngumu na wachezaji wenye uchu wa kufunga.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Asha Djafar (kushoto), akishangilia moja kati ya mabao mawili aliyofunga sambamba na mchezaji mwenza wa timu hiyo, Olaiya Barakat wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Garde Republicaine FC ya Djibouti kwenye mechi ya Ukanda wa Cecafa ya kuwania kufuzu Ligi ya Mabingwa Afrika, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **MPIGAPICHA WETU**

"Nimecheza na timu dhaifu ila wachezaji wangu wanapambana kutafuta matokeo mazuri, Garde Republicaine FC walicheza kwa kuzuia na kujazana kati, hivyo tukatumia wachezaji wa pembeni na kupata matokeo mazuri.

"Tumeanza vizuri mechi ya kwanza na tunaenda kufanyia kazi madhaifu yetu na kujiandaa na mechi ijayo dhidi ya She Corporates, kupata matokeo mazuri," alisema Nkoma.

Alisema wanapambana kujiandaa vizuri kwa michezo yao yote iliyopo mbele yao ili kuhakikisha wanatumia vizuri faida ya michuano hiyo kuchezwa nyumbani.

# Azam yajisifu suluhu Zesco

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutoka suluhu dhidi ya Zesco ya Zambia kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi juzi usiku, Klabu ya Azam imetamba kuwa kikosi chao kiko kamili kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, maarufu 'Zaka Zakazi', amesema haikuwa kazi rahisi hata kidogo kupata suluhu dhidi ya timu ngumu ya Zesco.

"Mechi imeisha kikubwa na kama uliona mpira umeisha tulikuwa tunawashambulia wapinzani wetu na hii inaonyesha kuwa tulikuwa tuko vizuri na siyo unaisha golini kwako, unaonekana ilikuwa tia maji tia maji.

Haikuwa kazi ndogo, Zesco siyo timu rahisi hata kidogo, ni timu iliyofanikiwa sana, imewahi kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ingawa Zambia haikuchukua ubingwa msimu huu, lakini kwa miaka 10 iliyopita wamechukua ubingwa mara saba. Na hata yenyewe inaanzia raundi ya kwanza kwenye Kombe la Shirikisho, kwa hiyo tulikutana watu wa raundi ya kwanza," alisema Zaka Zakazi.

Kuhusu Ligi Kuu Tanzania Bara iliyoanza jana, alisema walishajiandaa siku ya kwanza tu Ligi Kuu msimu uliopita ilipomalizika.

"Tumeshajipanga, tulijipanga siku moja tu baada ya Ligi Kuu iliyopita kumalizika. Tulianza kutambulisha wachezaji mapema. Tumemsajilia kocha wetu wachezaji ambao anawahitaji kwa sifa ambazo alikuwa anazihitaji, tukajiandaa tukaenda hadi Misri, cha kufanya hapa ni kurekebisha mapungufu ambayo yameonekana kwenye mechi yetu dhidi ya Zesco," alisema.

Wakati kesho Azam ikifungua utepe wa Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Azam Complex, Zakazi alisema inaichukulia kwa uzito mechi hiyo kwa sababu ni timu ambayo inawasumbua sana kila wanapocheza nao.

"Msimu uliopita tulitoka nao sare hapa, halafu tukaenda kwao wakatufunga, kwa hiyo hatutaki kabisa hilo litokee tena msimu huu," alisema Ofisa Habari huyo.

# Michezo

Jumanne Agosti 16, 2022
Nipashe



## Bruyne atarajia Silva kubaki City




Kambole Phiri

# Yanga: Ni ushindi tu leo

## ●●●Nabi asema wamejipanga kuanza vizuri kutetea ubingwa kwa kuinyosha Polisi Tanzania, lakini...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Yanga kikiwasili salama jijini Arusha jana tayari kuanza kutetea taji lao la Ligi Kuu Bara kitakaposhuka Uwanja wa Sheikh Amri Abeid leo kuivaa Polisi Tanzania, Kocha Mkuu wa mabingwa hao, Nasreddine Nabi, amesema wamejipanga vizuri kuanza kwa ushindi.

Ligi Kuu Bara ilianza kutimua vumbi jana kwa michezo miwili kuchezwa ambapo Ihefu fc ilikuwa nyumbani Mbarali kuikaribisha Ruvu Shooting huku Namungo ikiwa mwenyeji wa Mtibwa Sugar mkoani Lindi.

Mbali na mchezo wa Polisi Tanzania dhidi ya Yanga, leo pia kutapigwa mechi nyingine ya ligi hiyo ambapo Singida Big Stars itakuwa nyumbani Uwanja wa Liti kuikaribisha Tanzania Prisons ya Mbeya.

Akizungumza na Nipashe jana kuelekea mechi hiyo, Nabi alisema licha ya kuhitaji muda zaidi wa kukisuka kikosi chake, lakini amejipanga vizuri kupata matokeo mazuri katika mchezo wao wa leo dhidi ya Polisi Tanzania.

"Nimefanyia kazi mapungufu ya kikosi changu, tuko tayari kwa ajili ya kuanza kampeni yetu ya kusaka pointi muhimu katika mchezo wa kesho (leo), wapinzani wetu ni wazuri tunahitaji kupata matokeo mazuri katika mchezo huo," alisema Nabi.

Alisema ataendelea kukisuka kikosi chake kadri wanavyokabiliana na mechi za ligi hiyo ili kuwa cha ushindani zaidi kuweza kupata matokeo mazuri na kufikia malengo yao ya kutetea ubingwa.

Kikosi cha Yanga ambacho kimetoka kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Simba katika mchezo wa Ngao ya Jamii Jumamosi, kiliwasili jana jijini Arusha kikiwa bila nyota wake watatu, Yussuf Athuman, Crispin Ngushi na Shaibu Abdallah (Ninja).

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Simba kuikaribisha Geita Gold katika Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati Dodoma Jiji FC ikiwa na shughuli pevu kwenye Dimba la Liti mkoani Singida dhidi ya Mbeya City.

Mechi nyingine zitakazopigwa kesho kukamilisha mzunguko wa kwanza ni kati ya Azam FC dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Azam Complex, Chamanzi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, huku Coastal Union ikiwa mwenyeji wa KMC FC.

## Phiri na Kambole watatisha - Kocha

**Na Adam Fungamwango**

MASTRAIKA Moses Phiri wa Simba na Lazarous Kambole wa Yanga, wametabiriwa kufanya makubwa kwenye Ligi Kuu ya Tanzania kama watapewa nafasi katika klabu zao licha ya kutocheza kwenye mechi ya Ngao ya Jamii Jumamosi iliyopita.

Kocha Msaidizi wa zamani wa Yanga, Noel Mwandila amesema kuwa moja ya usajili bora ambao umefanywa na klabu hizi kubwa ni kuwasajili wachezaji hao kwa sababu anawafahamu na ana uhakika watakuja kuwa msaada mkubwa kwenye klabu zao na kuzungumzwa kwenye Ligi Kuu ya Tanzania.

Mwandila ambaye alikuja nchini na kikosi cha Zesco, akiwa mmoja wa watu wa kwenye benchi la ufundi, alisema hakuwaona wachezaji hao kwenye mechi ya Ngao ya Jamii iliyochezwa Agosti 13 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwa sababu hawakucheza, lakini ndiyo kwanza ligi inaanza, hivyo anatarajia watakapopata nafasi wataonyesha kile walichonacho.

"Si kwa sababu hakufanya vema Kaizer Chiefs, ndiyo na Yanga hatofanya vema, hapana, huu ni mpira, hauko hivyo, Kambole atafanya vizuri kwa sababu namfahamu, Phiri hata msimu uliopita alikuwa bora kwenye Ligi Kuu ya Zambia, naye naamini ni suala la muda tu, atafanya vema," alisema Mwandila raia wa Zambia.

Kuhusu ubingwa wa Tanzania Bara alisema pamoja na kuangalia mechi ya 'dabi', timu yake ya zamani ya Yanga ikishinda mabao 2-1, lakini hawezi kutabiri nani anaweza kutwaa ubingwa au yeye kumpa nafasi kwa sababu timu zote ni nzuri, badala yake aliweka wazi kuwa kuna makosa madogo madogo ambayo yanahitaji kurekebishwa kwa pande zote.

"Yeyote anaweza kuchukua ubingwa," alisema.

Wachezaji hao wote ni wapya kwenye vikosi hivyo, Kambole akisajiliwa na Yanga kutoka Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, huku Phiri akisajiliwa na Simba kutoka Zanaco ya Zambia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >